


# KURUDI KWA UBABE WA KIDIJITALI

## Kuzimwa kwa mitandao mnamo mwaka 2021

#KeepItOn

# #KeepItOn

Kampeni ya #KeepItOn inaleta pamoja mashirika ya kimataifa na juhudi za kukomesha uzimaji wa mtandao. Kampeni hii ilizinduliwa na muungano wa takribani mashirika 70 mnamo mwaka 2016 katika RightsCon huko Silicon Valley. Uanachama wa muungano huo umeongezeka kwa kasi kufikia mashirika 282 kutoka nchi 105 duniani kote kuanzia mashirika ya kiraia, mashirika ya kutetea haki, na vikundi vya ushawishi hadi vituo vya utafiti, mitandao ya utambuzi, taasisi na mashirika ya vyombo vya habari.

Ripoti hii ni chapisho la Access Now kwa niaba ya #KeepItOn iliyoandikwa  na Marianne Díaz Hernández na Felicia Anthonio kwa ushirikiano na timu ya Access Now.

Waandishi wangependa hasa kuwashukuru Sage Cheng, Donna Wentworth, Ángela Alarcón, Bridget Andere, Golda Benjamin, Raman Jit Singh Chima, Marwa Fatafta, Natalia Krapiva, Namrata Maheshwari, Peter Micek, Kassem Mnejja, Wai Phyo Myint, Melody Patry, Dhevy Sivaprakasam, Alexia Skok, Carolyn Tackett, na Anastasiya Zhyrmont kwa michango yao. Wangependa kuwashukuru Data4Change, Software Freedom Law Center India (SFLC.in), Yodet, Miaan Group, Internet Outage Detection & Analysis (IODA), Athan, Kentik, Beam Reports, Open Observatory of Network Interference (OONI) na wanachama wengineo wa muungano wa #KeepItOn kwa kutoa taarifa muhimu na maarifa kuhusu tafiti, kukagua data na vyanzo na kuchangia ripoti.

Ubunifu na taswira ya data imefanywa na Sage Cheng.

## Ujumbe juu ya data yetu

Ripoti hii ya #KeepItOn inaangazia matukio ya uzimaji wa mtandao yaliyorekodiwa na Access Now na muungano wa #KeepItOn mnamo mwaka 2021. Ingawa tunajaribu kuunda hifadhidata ya kina, data yetu inategemea vipimo vya kiufundi na pia maelezo yanayohusishsa muktadha, kama vile ripoti za habari au akaunti za kibinafsi. Vikwazo vya mbinu zetu vinamaanisha kuwa kunaweza kuwa na visa vya kuzimwa kwa mitandao ambavyo havijaripotiwa na nambari zinaweza kubadilika ambapo habari mpya zitapatikana baada ya kuchapishwa. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea https://accessnow.org/keepiton-data-methodology.

Aprili 2022

CC BY

# Table of Contents


**I. Kuzimwa kwa mitandao mnamo 2021: Mukhtasari wa kimataifa** 2

1.1 Kuangazia kuzimwa kwa mtandao kikanda na kwa nchi maalum 6

Afrika 6

Asia ya Pasifiki 7

Ulaya Mashariki na Asia ya Kati 8

Amerika ya Kusini na Karibiani 11

Mashariki ya Kati na Afrika ya Kaskazini 11

**II. Vichochezi vya kuzima kwa mtandao mnamo 2021** 13

2.1 Kuzimwa kwa mitandao wakati wa maandamano, misukosuko ya kisiasa na mapinduzi 15

Mapinduzi ya Myanmar 15

Mapinduzi ya Sudani 15

Ukandamizaji mbaya wa Irani dhidi ya maandamano 16

Nchi nyingine zilizo kwenye uangalizi 16

2.2 Kuzimwa kwa mitandao wakati wa uchaguzi 17

Jinsi muungano wa #KeepItOn unavyoitikia 19

2.3 Kuzimwa kwa mitandao katika maeneo ya migogoro 20

Ethiopia: Kukatika kwa intaneti huko Tigray kunaongeza athari za vita vya kikatili vya wenyewe kwa wenyewe 21

Mashambulizi ya Israel kwenye Ukanda wa Gaza 22

Mapinduzi ya kidijitali ya jeshi la Myanmar yanayoendelea 23

2.4 Kuzimwa kwa mitandao nyakati za mitihani 24

**III. Mitindo na maendeleo mashuhuri katika 2021** 25

3.1 Kuzima mitandao kwa muda mrefu 25

3.2 Kuongezeka kwa matumizi ya kuzima kwa simu wakati wa maandamano 25

3.3 Uzuiaji unaolengwa wa majukwaa ya mawasiliano 26

3.4 Teknolojia zinazoendelea: kuchanganya kubana, kuzuia na kuzimwa kwa mitandao 28

3.5 Kuzimwa mitandao kwa kulenga kwa maeneo na ya watu maalumu 28

**IV. Kupambana katika mwaka 2021: changamoto na fursa** 29

4.1 Hatua zilizopigwa katika ngazi za kimataifa 29

4.2 Hatua Zilizopigwa mahakamani za kupinga kuzimwa kwa mitandao 30

4.3 Maendeleo ya kuwezesha asasi za kiraia kukwepa na kupinga kuzimwa kwa mitandao 31

4.4 Maendeleo ya ufuatiliaji shirikishi na uchanganuzi wa kuzimwa kwa mitandao 32

**V. Hitimisho: harakati zetu zinahitaji kuendelea kukua** 32

# I. Kuzimwa kwa mitandao mnamo 2021: Mukhtasari wa kimataifa


Tunaporejelea hali ya kawaida kufuatia kuzuka kwa janga la kimataifa la COVID-19, tuliona kuzuka tena kwa kasi kwa kuzimwa kwa mitandao mnamo 2021.[1] Katika mwaka huu, Access Now pamoja na #KeepItOn ilirekodi angalau matukio **182** ya uzimaji wa mitandao duniani kote katika nchi **34**, ikilinganishwa na angalau matukio **159** ya uzimaji wa mitandao katika nchi **29** mwaka 2020. Tumeona ongezeko la kimataifa la kuzimwa kwa mitandao kwa matukio **23** kutoka mwaka 2020 hadi mwaka 2021.

Kufuatia mienendo ambayo tumeona ikiendelezwa kwa miaka mingi, mwaka 2021 serikali ziliweka vikwazo vya muda mrefu na vilivyolenga zaidi intaneti na kutegemea sababu nyingi sawa za kupelekea hatua hizi kali zisizo na uwiano. Mamlaka katika nchi nyingi zilizima mitandao katika juhudi za uwazi za kunyamazisha wakosoaji na kukandamiza upinzani. Nyingine zilizima mitandao ili kudhibiti mtiririko wa taarifa wakati wa uchaguzi na mizozo na vita, ikiwa ni pamoja na mapinduzi. Katika baadhi ya matukio, nchi ziliendelea na mazoea mabaya ya kutatiza ufikiaji wa miandao wakati wa mitihani ya shule, njia ya dharura ya kuzuia udanganyifu.

India iliwajibika kwa matukio **106** ya kuzima mitandao kwa kumbukumbu za mnamo mwaka 2021, na kuifanya kuwa muhalifu mkubwa zaidi ulimwenguni kwa mwaka wa nne mfululizo. Baada ya India, Myanmar ilisajili idadi kubwa zaidi ya kuzima mitandao mnamo mwaka 2021, na kuzima mara **15**, ikifuatiwa na Sudani na Irani zote mbili zikizima mtandao mara **tano**. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, nyaraka zetu zinaonyesha kuwa mamlaka zimezidi kuzima mitandao ya intaneti wakati wa matukio yanayoathiri hali ya kisiasa nchini, kama vile uchaguzi, maandamano, mapinduzi na migogoro mikali. Hasa, nchi **saba**

1 Kuzimwa kwa mtandao kumefafanuliwa kama "kukatizwa kimakusudi kwa mtandao au mawasiliano ya kielektroniki na kufanya zisifikiwe au zisitumike ipasavyo kwa watu mahususi au ndani ya eneo, mara nyingi ili kudhibiti mtiririko wa habari." Kuzimwa kwa mtandao hutokea wakati mtu - kwa kawaida serikali - inakatiza programu za intaneti au simu kwa makusudi ili kudhibiti kile ambacho watu husema au kufanya. Access Now (n.d.) Imerudiwa Machi 30, 2021, kutoka kwenye https://www.accessnow.org/keepiton-faq/

## Idadi iliyosajiliwa ya kufungwa kwa mitandao kwa kila nchi




## Idadi za nchi zinazozima mitandao

**34** Nchi mwaka wa 2021

**29** Nchi mwaka wa 2020

**33** Nchi mwaka wa 2019

**25** Nchi mwaka wa 2018

* Hizi namba zatokana na utafiti wa mwisho uliofanywa.katika ripoti hii. Utafiti uliopita umeongezwa hapa pamoja na matokeo mapya yaliyopatikana.

## Athari ya UVIKO-19

# Siku 2026

Kuanzia 2016 hadi 2021, wakazi 4.5 milioni wa eneo la kikabila la FATA, walifungiwa intaneti kwa hiyo miaka mine takriban. Hili lilikaribia kuua elimu, huduma za kiafya, matibabu, na furssa za kibiashara kwa uma ambao ulikuwa tayari ushatengwa, hususan kwa kipindi cha janga la UVIKO-19.

# Mara 15

Viongozi wa kijeshi wa Myanmar walifunga mitandao mara 15 mwa kwa wa 2021. Muda mrefu zaidi wa mtandao kufungwa nchini humo, ulichukua takribanmiezi miwili na nusu..

# Miezi 18

Nchini Ethiopia, wakazi wa Tigray walikatiwa mtandaotangu 2020, ambao ni muda wa miezi 18 na bado yaendelea.

# Mara 85

Wakazi wa Jammu na Kashmir, katika mwaka wa 2021 walifungiwa mitandao mara 85. Sababu kubwa ya kufungwa ilidaiwa kuwa ni vita dhidi ya ugaidi. Hii ilisababisha Bonde la Kashmir kukamilisha mwaka mzima bila ya mitandao.

kwenye rekodi yetu ambazo hazijawahi kuzima mitandao kabla ya kujiunga na orodha ya aibu mwaka wa 2021: Burkina Faso, Niger, Palestina, Senegal, Sudani ya Kusini, Eswatini (zamani Swaziland) na Zambia. Kwa upande mwingine, katika maendeleo chanya, nchi zikiwemo Benini, Iraqi na Gambia, ambazo hapo awali zilikuwa zimezima mitandao wakati wa matukio muhimu ya kitaifa, ziliwachilia mitandao kuwa wazi wakati wa uchaguzi wa mwaka 2021.

Ukituzia makini data za mwaka 2021 unaonyesha kwamba kile ambacho kingeliweza kuwa hadith nzurii juu ya kupungua kwa kasi ya kuzimwa kwa mitandao baada ya janga hilo badala yake inaonyesha kurudi kwa mbinu za kudhuru haki za kipindi cha kabla ya janga. Na mbinu hizi zinaenea. Hilo linakera hasa kutokana na ambavyo tunaendelea kutegemea mtandao ili kuwa salama na wenye afya, kuungana na wapendwa wetu na kushiriki kikamilifu katika ulimwengu wa kisasa wa kidijitali.[2] Pia ni ishara nyingine ya onyo ya **kuongezeka kwa ubabe wa kidijitali** kote ulimwenguni.[3]

Mnamo mwaka 2021, tuliona kuzimwa kwa mitandao katika maeneo yenye migogoro na kama aina ya mashambulizi katika migogoro, ikiwa ni pamoja na kabla, wakati na baada ya mapinduzi mawili (Myanmar na Sudani). Kuzimwa kwa mitandao huko Yuropa Mashariki na Asia ya Kati, pamoja na Urusi kunaonyesha mvutano wa kisiasa za kijiografia ambao tunaona ukilipuka leo. Mwenendo unaoendelea wa kuzima mitandao kwa muda mrefu (nchini Ethiopia, Myanmar, India, Pakistani, na kwingineko) ni kiashiria cha kuhuzunisha cha nia ya mamlaka za kiserikali kutenganisha na kuongeza mateso ya watu wao wenyewe.

Tunapoangalia kuanza tena kwa kuzimwa kwa mitandao mnamo mwaka 2021, ni athari ya kibinadamu ambayo ni muhimu zaidi. Kukatizwa kwa mitandao kunaweza kusababisha ukiukaji wa haki za kibinadamu[4] wakati wa migogoro, ikiwa ni pamoja na uhalifu wa kivita na

2 Pew Research Center: Internet, Science & Tech (2021). *Mtandao na janga.* Imerejeshwa Januari 14, 2022, kutoka https://www.pewresearch.org/internet/2021/09/01/the-internet-and-the-pandemic/.

3 Deutsche Welle (2022). *Ubabe wa kidijitali: Jambo la kimataifa.* Imerejeshwa Aprili 6, 2022 kutoka https://www.dw.com/en/digital-authoritarianism-a-global-phenomenon/a-61136660

4 ARTICLE 19 (2021). *Iran: Internet shutdowns curb protests and conceal human rights violations in Sistan and Baluchistan.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.article19.org/resources/iran-internet-shutdowns-curb-protests-and-conceal-human-rights-violations-in-sistan-and-baluchistan/.

mauaji ya kimbari.[5] Hayo yanazuia na kutatiza misaada ya kibinadamu,[6] na kuzuia uandishi wa habari na uwekaji kumbukumbu wa ukiukaji wa haki.[7] Pia huwaacha watu ambao wana wapendwa wao katika maeneo haya yenye mizozo wakiwa na hofu, wasiweze kufikia familia na marafiki au kuwafikisha mahali salama. Nchini Myanmar, kwa mfano, kuzimwa kwa mitandao kumezuia uwezo wa kuripoti mashambulizi ya anga dhidi ya raia, kuchomwa kwa nyumba, na mauaji ya kiholela na kukamatwa, ikiwa ni pamoja na watoto.[8]

Bila kujali muktadha au mantiki, kuzimwa kwa mitandao ni shambulio dhidi ya haki za binadamu. Janga la kimataifa la COVID-19 limeangazia tu ukali wa kuwatenganisha watu kutoka kwenye mitandao wakati unatumiwa kwa kila kitu kuanzia upatikanaji wa elimu, kazi na huduma za benki, kufikia habari, utamaduni na burudani, na vilevile mawasiliano ya kimsingi nchini katika maisha ya kila siku.[9]

Ni matumaini yetu kuwa ripoti hii itatumika kama onyo: **puuza kuzimwa kwa mitandao kwa hatari yako**. Kamwe si ishara ya kuheshimu haki za binadamu, demokrasia yenye afya au utawala bora.

**Idadi ya kufungwa kwa mitandao kwa kila nchi kufikia mwaka wa 2021**



**India:** 106
**Myanmar:** 15
**Irani:** 5
**Sudani:** 5
**Cuba:** 4
**Jordani:** 4
**Ethiopia:** 3
**Uganda:** 3

**Bangladesh:** 2 **Chadi:** 2 **Eswatini:** 2 **Indonesia:** 2 **Iraqi:** 2 **Kazakhstani:** 2 **Nigeria:** 2 **Pakistani:** 2 **Syria:** 2 **Turkmenistani:** 2 **Yemen:** 2

**Afghanistani:** 1 **Algeria:** 1 **Burkina Faso:** 1 **China:** 1 **Jamhuri ya Kongo:** 1 **Gaboni:** 1 **Niger:** 1 **Omani:** 1 **Palestina:** 1 **Urusi:** 1 **Senegal:** 1 **Sudani ya Kusini:** 1 **Tajikistani:** 1 **Uzbekistani:** 1 **Zambia:** 1

5 Freedom House (2021). *Freedom on the Net 2021 - Myanmar.* Imerejeshwa Aprili 17, 2022, kutoka https://freedomhouse.org/country/myanmar/freedom-net/2021

6 Reinventing Peace (2021). *Switch Tigray's Internet Back On.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://sites.tufts.edu/reinventingpeace/2021/04/21/switch-tigrays-internet-back-on/.

7 WITNESS (2021). *#Eyesonshutdowns: Documenting for human rights.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.witness.org/eyesonshutdowns-documenting-for-human-rights/.

8 Myanmar Now (2022). *Myanmar junta cuts off internet access 'indefinitely' to resistance stronghold of Sagaing*. Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.myanmar-now.org/en/news/myanmar-junta-cuts-off-internet-access-indefinitely-to-resistance-stronghold-of-sagaing; The Irrawaddy (2022). *Sagaing Region Internet Shut Down Amid Myanmar Junta Raids.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.irrawaddy.com/news/burma/sagaing-region-internet-shut-down-amid-myanmar-junta-raids.html.

9 Access Now (2021). *Cutting internet access when people need it the most: stories from Uganda.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/internet-shutdown-stories-from-uganda/.

**Kufungwa kwa mtandao kwa kila sehemu mwaka wa 2021**

Cuba: 4

Amerika ya Kusinini na Karibiani


- Afrika: Ilifungwa mara 19 katika nchi 12 mwaka wa 2021 ikilinganishwa na mara 19 katika nchi tisa mwaka wa 2020.
- Asia Ya Pasifiki: Ilifungwa mara 129 katika nchi 7 mwaka wa 2021 ikilinganishwa na mara 114 katika nchi tano mwaka wa 2020.
- Yuropa Mashariki na Asia Ya Kati: Ilifungwa mara saba katika nchi 5, mwaka wa 2021 ikilinganishwa na mara 4 katika nchi tatu mwaka wa 2022.
- Amerika Kusini na Karibiani: Ilifungwa mara nne katika nchi moja mwaka wa 2021 ikilinganishwa na mara nne katika nchi tatu mwaka wa 2022.
- Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini: Ilifungwa mara 23 katika nchi 9 mwaka wa 2021, ikilinganishwa na mara 18 katika nchi tisa mwaka wa 2022.

## 1.1 Kuangazia kuzimwa kwa mtandao kikanda na kwa nchi maalum

### Afrika

Mnamo mwaka 2021, nchi **12** zilikata ufikiaji wa mtandao mara **19** barani Afrika, nchi **tatu** zaidi kuliko mwaka uliopita. Ni nini kinachosababisha kuenea kwa usumbufu wa mitandao barani Afrika? Jamhuri ya Kongo, Chadi, Niger, Uganda na Zambia zilifanya uchaguzi mwaka 2021, na kulikuwa na maandamano na machafuko makubwa ya wenyewe kwa wenyewe huko Eswatini, Ethiopia, Gaboni, Senegal na Sudani ya Kusini.[10] Chaguzi na maandamano ni vichocheo vya kawaida vya kuzimwa kwa mtandao Afrika na kote ulimwenguni, kwani mamlaka huitumia kushurutisha au kudumisha udhibiti wa watu, kwa kuathiri haki za kimsingi za raia na uhuru wa kidemokrasia. Tawala dhalimu na za kimabavu pia hujifunza kutoka kwa mataifa ya kidikteta kama yao, zikiiga mbinu za kudhuru haki ili kudhibiti hali.

Mfano mmoja wa kuzimwa kwa mitandao barani Afrika ambao unaachana na mtindo huu wa ghiliba kwa ajili ya udhibiti wa kisiasa ni kuzimwa kwa mitandao nchini Nigeria iliyoamrishwa kukabiliana na kile kinachojulikana nchini huko kama ujambazi, ikimaanisha magenge ya wahalifu wanaotekeleza utekaji nyara, wizi wa ng'ombe na uhalifu mwingine. Kulingana na ripoti ya habari, maafisa walikatiza kwa muda huduma za mawasiliano ya simu katika baadhi ya majimbo ya Zamfara na Kaduna kwa sababu magenge hayo yalikuwa yanazitumia kutahadharishana kuhusu eneo la wanajeshi wa serikali. [11]




10 Access Now (2021). *#KeepItOn: 2021 Elections Watch*. Imerejeshwa Januari 12, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/keepiton-2021-elections-watch/.

11 Fin24 (2021). *Nigeria cuts cellphone network in tense northern state.* Imerejeshwa Februari 28, 2022, kutoka https://www.news24.com/fin24/international/nigeria-cuts-cellphone-network-in-tense-northern-state-20210905.


## Asia ya Pasifiki

Mnamo mwaka 2021, tulirekodi jumla ya matukio **129** ya kuzimwa kwa mitandao katika nchi saba za Asia ya Pasifiki, ikilinganishwa na kuzimwa mara **114** katika nchi **tano** mwaka 2020.

**India** ilisababisha matukio **106**, na kuifanya kuwa nchi yenye idadi kubwa zaidi ya kuzima mitandao ulimwenguni kwa mwaka wa nne mfululizo. Kati ya haya, matukio **85** ilikuwa Jammu na Kashmir, eneo ambalo mamlaka inaendelea kuweka usumbufu wa kukusudia wa mitandao ambao hudumu kwa muda mrefu, unaovuruga na kuhatarisha maisha ya watu kwa miezi kadhaa.

Kwa bahati mbaya, inawezekana kwamba tunakosa pia fursa ya kusajili usumbufu fulani wa mitandao ambao ulifanyika kwa sababu ya ukosefu wa uwazi wa serikali. Serikali ya India imekuwa ikisita kuunda na kudumisha hazina kuu ya data juu ya agizo la mamlaka ya kuzima huduma ya mitandao kote nchini.[12] Hii inawakilisha kushindwa kukidhi mahitaji ya Kanuni za Kusimamishwa za mwaka 2017 na amri ya Mahakama ya Juu inayoziunga mkono.[13] Ukosefu wa hazina kuu inaendelea kufanya kuwa vigumu kwa mashirika ya kiraia na wadau wengine kufuatilia kwa ufanisi na kuweka kumbukumbu na baadhi yao huenda yasiripotiwe.

Vizuizi vilivyowekwa na mamlaka ya India mnamo mwaka 2021 vilivuta hisia za kimataifa na kulaaniwa. Serikali ilikata ufikiaji wa mtandao katika jaribio la wazi la kukandamiza Maandamano ya Wakulima, harakati inayopinga Bunge la India kupitisha sheria tatu za kilimo mwaka uliopita.[14] Mamlaka zilitaka kwa uwazi kuwazuia waandamanaji wasiwasiliane wao kwa wao, na kuzuia kuripoti kwenye vyombo vya habari. Licha ya usumbufu huo, serikali haikuweza kuficha ukandamizaji wake mkali dhidi ya wapinzani




12 Government of India (2022). *Internet shutdowns.* ImerejeshwaMachi 18, 2022, kutoka http://164.100.24.220/loksabhaquestions/annex/178/AU1305.pdf.

13 Home: Department of Telecommunications: Ministry of Communication: Government of India (2017). Imerejeshwa Februari 27, 2022, kutoka https://dot.gov.in/circulars/temporary-suspension-telecom-services-public-emergency-or-public-safety-rules-2017

14 The New York Times (2021). *What Prompted the Farm Protests in India?* Imerejeshwa Machi 13, 2022, kutoka https://www.nytimes.com/2021/01/27/world/asia/india-farmer-protest.html.

na waandamanaji halali[15] na serikali za ulimwengu [16] na watu mashuhuri wa kimataifa Greta Thunberg na Rihanna walizungumza dhidi ya ghasia na usumbufu wa makusudi.[17]

Kuzimwa kila mara kwa mitandao nchini India licha ya malalamiko na kanuni za kimataifa zinazohitaji uwazi zaidi kunamaanisha kuwa hakujawa na uboreshaji mwingi wa hali hiyo. Serikali iliendelea kushurutisha kuzima mtandao wakati wa maandamano, na iliendelea kufuata vizuizi vya muda mrefu ambavyo vinaacha watu kukatiwa mitandao wakati tu wanahitaji kubwa la kuunganishwa.[18]

Mnamo Desemba 2021, Kamati ya Kudumu ya Bunge la India kuhusu Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ilitoa ripoti[19] inayoangazia matumizi mabaya ya kuzimwa kwa mtandao, na athari yake kwa haki na uhuru, na kutoa mapendekezo kwa serikali kurekebisha mfumo unaosimamia kusimamishwa kwa huduma za mawasiliano/mtandao. Ingawa ripoti inatoa mapendekezo kadhaa chanya yanayolenga kuimarisha uwazi na uwajibikaji, na kuimarisha ulinzi, hailaani kabisa matumizi ya kuzima kwa mtandao na inashindwa kutaja ukweli mmoja muhimu zaidi wa kuzimwa kwa mtandao: kamwe haiwezi kukubalika kuwa ya haki na usawa.

Ilikuwa ni mwaka 2021 ambapo jeshi la Myanmar lilitekeleza mapinduzi yake,[20] na nchi hiyo inaifuata India kwenye orodha ya aibu, na kuweka idadi ya pili ya juu ya usumbufu duniani, na angalau matukio **15** ya kuzimwa kwa mitandao. Idadi hii ina uwezekano wa chini kuliko idadi halisi matukio ya kuzima mitandao, kutokana na kunyakua udhibiti wa jeshi na migogoro inayoendelea. Nchini Afghanistani, pia eneo ambalo lilikuwa na migogoro mnamo mwaka 2021, Talibani ilifunga ufikiaji wa mitandao pamoja na miunganisho ya simu na aina zingine za mawasiliano katika mkoa wa Panjshir ili kupunguza upinzani kutoka kwa eneo hilo.[21]

## Ulaya Mashariki na Asia ya Kati

Kuzimwa kwa mitandao kunaweza kuwa ishara ya onyo ya ubabe, na dalili kwamba demokrasia inashambuliwa.[22] Tuliyoyaona mwaka 2021 katika Yuropa Mashariki na Asia ya Kati yanaonekana kwa kuzingatia nyuma ili kuashiria majaribio makali ya mamlaka ya serikali ya kutaka kudhibiti watu, huku ukaguzi mkubwa na usumbufu wa mtandao ukiweka msingi wa uvamizi wa siku zijazo.[23]

Mnamo Februari 28, 2021, mamlaka nchini Kazakhstani iliweka vikwazo vya mtandao katika miji ya Almaty na Nur-Sultan ili kuzima maandamano ya kupinga serikali ya kutaka wafungwa wa kisiasa waachiliwe.[24] Kulikuwa na ripoti za ghasia na mamlaka iliwazuia waandamanaji wasiopungua 50.[25] Kwa

15 Internet Freedom Foundation (2021). *Joint statement against internet shutdowns to suppress farmers' protests #KeepItOn.* Imerejeshwa Machi 18, 2022, kutoka https://internetfreedom.in/joint-statement-internet-shutdown-farmers-protests/.

16 The Wire (2021). *Farm Laws: US Says Access to Internet, Peaceful Protests Are 'Hallmarks of a Thriving Democracy.'* Imerejeshwa Machi 22, 2022, kutoka https://thewire.in/diplomacy/farm-laws-us-says-access-to-internet-peaceful-protests-are-hallmarks-of-a-thriving-democracy; Scroll.in (2021). *Farmer protest shows need for consultations on laws with those concerned, says UN human rights chief.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://scroll.in/latest/988064/farmer-protest-shows-need-for-consultations-on-laws-with-those-concerned-says-un-human-rights-chief

17 The Logical Indian (2021). *Farmers' Protest Gets Global Attention, Rihanna, Greta Thunberg Tweet In Support Of Farmers.* Imerejeshwa Februari 18, 2022, kutoka https://thelogicalindian.com/trending/farmers-protest-rihanna-greta-thunberg-26604.

18 International Journal of Asian Business and Information Management (IJABIM) (2021). *How Internet Shutdowns Affects the Entrepreneurs in Jammu and Kashmir.* Imerejeshwa Januari 31, 2022, kutoka https://www.igi-global.com/article/how-internet-shutdowns-affects-the-entrepreneurs-in-jammu-and-kashmir/279813.

19 Ministry of Communications (2021). *Standing Committee on Communications and Information Technology*. Imerejeshwa Aprili 20, 2022,kutoka http://164.100.47.193/lsscommittee/Communications%20and%20Information%20Technology/17_Communications_and_Information_Technology_26.pdf.

20 Access Now (2021). *Update: internet access, censorship, and the Myanmar coup.* Imerejeshwa Januari 28, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/update-internet-access-censorship-myanmar/.

21 Daily Beast (2021). *This Is Why the Taliban Keeps F*cking Up the Internet.* Imerejeshwa Aprili 21, 2022, kutoka https://www.thedailybeast.com/this-is-why-the-taliban-keeps-fcking-up-afghanistans-internet.

22 Freedom House (2018). *The Rise of Digital Authoritarianism.* Imerejeshwa Aprili 5, 2022, kutoka https://freedomhouse.org/report/freedom-net/2018/rise-digital-authoritarianism.


23 Al Jazeera (2022). *Russian forces launch full-scale invasion of Ukraine*. Imerejeshwa Machi 21, 2022, from https://www.aljazeera.com/news/2022/2/24/putin-orders-military-operations-in-eastern-ukraine-as-un-meets.

24 Access Now (2021). *Civil society reports internet shutdowns in two cities in Kazakhstan during February 28 protests.* Imerejeshwa Machi 31, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/internet-shutdowns-kazakhstan-feb-28-protests/.

25 Rus.azattyg.org (2021). *February 28 in Kazakhstan: "kettling", "titushki" and preventive detentions.* Imerejeshwa Februari 18, 2022, kutoka https://rus.azattyq.org/a/31126079.html.

**Maeneo na upeo wa kufungwa mitandao katika Ulaya Mashariki na Asia ya Kati mwaka wa 2021** ▼

**Daraja la 1: Iliathiri jiji moja, jimbo moja au kijiji.**
**Daraja la 2: Iliathiri zaidi ya jiji moja, ndani ya mkoa mmoja, jimbo moja au eneo**
**Daraja la 3: Iliathiri sehemu kwenye zaidi ya jimbo moja, mkoa mmoja, au eneo**
**Hali zisizojulikana: Haieleweki ni sehemu gani zilizoathirika**




kuzingatia juhudi zake za kudhibiti anga ya kidijitali nchini, serikali pia ilianzisha sheria ya kulazimisha makampuni ya kigeni ya teknolojia kuanzisha ofisi za ndani, zitakazoongozwa na raia wa Kazakh, na kufuta taarifa zozote za mamlaka ndani ya saa 24.[26]

Nchini Turkmenistani, mamlaka imewanyima watu ufikiaji wa majukwaa ya mitandao ya kijamii, vyombo vya habari vya kigeni na tovuti ambazo huandaa taarifa zinazokosoa utawala wa sasa kwa miaka mingi. Mnamo mwaka 2021, tuliona mamlaka ikiongeza udhibiti wa mtandaoni walipozuia tovuti zinazotoa zana za kukwepa kutambulika kama vile mitandao ya faragha ya mtandaoni (VPNs). Watu waliojiandikisha kupata muunganisho wa intaneti wa nyumbani walilazimika hata kuapa kwa Quran kutotumia zana za kukwepa kutambulika,[27] huku wanafunzi wakitakiwa kutoa matamko ya kuahidi kutumia intaneti kwa "madhumuni ya kielimu" pekee.[28] Hasa, kufikia Aprili 2022, mamlaka nchini Turkmenistani bado inawanyima watu ufikiaji wa huduma muhimu mtandaoni.[29]

Kwa bahati mbaya, mamlaka nchini Tajikistani ilifuata mtindo kama huo wa udhibiti usio na uwiano wa mtandaoni mwaka 2021. Katika mji wa Tajik ya Khorog, serikali ilizuia majukwaa ya mitandao ya kijamii kujibu maand amano na kuwalazimu watu kusafiri mamia ya kilomita hadi miji jirani ili kuunganishwa na mtandao.[30]

Wakati huo huo, nchini Uzbekistani, mdhibiti wa mawasiliano wa kitaifa alizuia ufikiaji wa tovuti nyingi za mitandao ya kijamii na maombi ya ujumbe wa papo hapo tarehe 3 Novemba 2021, akitoa mfano wa kutofuata sheria za ulinzi wa data.[31] Ripoti kutoka kwa Open Observatory of Network Interference (OONI) inaonyesha kuwa ufikiaji wa Facebook, Signal, WhatsApp, Facebook Messenger na Telegraph umerejeshwa, lakini hadi Machi 2022 watu bado hawakuweza kufikia Twitter, Vkontakte, TikTok, au Skype bila VPN.[32]

26 Access Now (2021). *Kazakhstan's plan of tech platform "localization" opens door to censorship.* Imerejeshwa Machi 31, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/kazakhstans-tech-platform-localization-censorship/.

The Times (2021). *Swear on the Quran to get connected.* Imerejeshwa Februari 18, 2022, kutoka https://www.thetimes.co.uk/article/swear-on-the-quran-to-get-connected-2ksvldnv0.

RadioFreeEurope/RadioLiberty (2021). *Turkmenistan Increases Crackdown On Internet Access As Living Standards Continue Downward Spiral.* Imerejeshwa Februari 18, 2022, kutoka https://www.rferl.org/a/turkmenistan-increases-crackdown-on-internet-access-as-living-standards-continue-downward-spiral/30846977.html.

29 ACCA (2022). *Turkmenistan: The authorities almost completely blocked the Internet in the country.* Imerejeshwa Aprili 19, 2022, kutoka https://acca.media/en/turkmenistan-the-authorities-almost-completely-blocked-the-internet-in-the-country/.

30 Plus (2021). *Drive 600 km in search of the Internet. Why is communication not available in GBAO and how do people suffer because of this?* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.asiaplustj.info/ru/news/tajikistan/security/20211207/proehat-600-km-v-poiskah-interneta-pochemu-ne-dayut-svyaz-v-gbao-i-kak-iz-za-etogo-stradayut-lyudi.

31 RadioFreeEurope/RadioLiberty (2021). *Uzbekistan Restricts Access To Most Social Media, Instant Messaging Sites.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.rferl.org/a/uzbekistan-social-media-restrictions/31544451.html.

32 OONI (2021). *Open Observation Network Interference.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://ooni.org/reports/; Eurasianet (2022). *Uzbekistan unblocks, re-blocks popular social media amid TikTok talks.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kuroka https://eurasianet.org/uzbekistan-unblocks-re-blocks-popular-social-media-amid-tiktok-talks.

Hatimaye, kuna Urusi, nchi pekee iliyozuia ufikiaji wa majukwaa ya mawasiliano katika Yuropa Mashariki mwaka wa 2021. Hatua za serikali zinaonyesha kuongezeka wazi kwa mbinu za udhibiti, kutoka kwenye udhibiti wa tovuti au mashirika fulani, ili kuondoa maagizo ya majukwaa makubwa ya mawasiliano ya mtandaoni hadi kuzorotesha (kuzifanya ziwe polepole) kwa majukwaa haya hadi vizuizi kamili vya jukwaa.

Mnamo Machi 2021, Roskomnadzor, wakala wa Urusi aliye na jukumu la kuhakikisha utiifu wa sheria za vyombo vya habari na mawasiliano ya simu, alijibu kukataa kwa Twitter kuondoa maudhui iliyoalamishwa kwa kuagiza makampuni ya mawasiliano kuzima ufikiaji wa jukwaa linalotumiwa sana. Uamuzi huo ulikuwa na matokeo yasiyotarajiwa[33] na kupunguza kasi ya kufikia zaidi ya vikoa 40,000 vilivyo na t.co (jina la kikoa lililofupishwa la Twitter). Hiyo ilijumuisha tovuti za taasisi muhimu za serikali nchini Urusi, pamoja na majukwaa makuu ya Google na Yandex.[34]

Udhibiti wa kasi ya mtandao ni miongoni mwa mbinu nyingi ambazo serikali ya Urusi imefuata kulazimisha makampuni ya kigeni ya teknolojia kufanya zabuni zake. Baada ya Google na Meta kukataa kuondoa maudhui ambayo serikali iliona kuwa kinyume cha sheria, mamlaka ya Urusi iliwasilisha mashtaka dhidi yao.[35] Pia waliwatishia wafanyakazi wa Google na Apple, na kufanikiwa kuzishawishi kampuni hizi kuondoa programu ya Smart Voting ya kiongozi wa upinzani Alexey Navalny kutoka kwenye maduka na majukwaa yao siku ya uchaguzi.[36] Mamlaka pia ilizuia VPN ili kuwazuia watu wa Urusi kukwepa udhibiti huu.[37]

Inaonekana juhudi za serikali zilizofanikiwa kudhibiti nafasi za kidijitali za Urusi zilitia nguvu mamlaka tu, na kuwatia moyo kwenda mbali zaidi. Baada ya Urusi kuivamia Ukraine mnamo Februari 2022, tumeona ukandamizaji mkubwa zaidi wa uhuru wa kujieleza huku serikali ikijaribu kukandamiza upinzani na kupata udhibiti wa simulizi kuhusu mzozo huo. Mamlaka imepitisha sheria mpya zinazozuia hotuba kuhusu vita na kupiga marufuku mifumo ya kidijitali na midia, pamoja na zana za kukwepa kutambulika[38] kama vile VPN. Baada ya Facebook kuamua kuwaruhusu kwa muda watu nchini Ukraine kuitisha vurugu dhidi ya wakuu wa nchi na wanajeshi wa Urusi wanaovamia nchi yao, mahakama ya Urusi ilitangaza kampuni mama ya Meta kuwa "yenye msimamo mkali," ikipiga marufuku kikamilifu matumizi ya mitandao ya Facebook na Instagram nchini Urusi.[39]

Inaaminika kuwa serikali ya Belarusi, ambayo ilikata ufikiaji wa mtandao[40] wakati wa vurugu za uchaguzi mnamo mwaka 2020 na sasa inasaidia Urusi kupigana vita nchini Ukraine,[41] ilichukua hatua mnamo mwaka 2021 kuweka nguvu zake za kupiga "mabadiliko ya kuua" na kuzuia ufikiaji wa mtandao kwa hiari yake.[42]

33 Access Now (2021). *Russia throttled Twitter to censor content — Here's what happens next.* Imerejeshwa Februari 18, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/russia-throttled-twitter/.

34 WIRED (2021). *Russia's Failure to Throttle Twitter Isn't a Sign of Weakness.* Imerejeshwa Machi 21, 2022, kutoka https://www.wired.com/story/opinion-russias-failure-to-throttle-twitter-isnt-a-sign-of-weakness/.

35 The Moscow Times (2021). *Russia Fines Google for Failing To Remove Banned Content.* Imerejeshwa Machi 21, 2022, kutoka https://www.themoscowtimes.com/2020/12/17/russia-fines-google-for-failing-to-remove-banned-content-a72400.

36 The New York Times (2021). *Google and Apple, Under Pressure From Russia, Remove Voting App.* Imerejeshwa Machi 22, 2022, kutoka https://www.nytimes.com/2021/09/17/world/europe/russia-navalny-app-election.html.

37 Roskomnadzor (2021). *Federal Service for Supervision of Communications, Information Technology and Mass Communications.* Imerejeshwa Machi 22, 2022, kutoka https://rkn.gov.ru/news/rsoc/news73836.htm.

38 POLITICO (2022). *Russia expands laws criminalizing 'fake news'.* Imerejeshwa Aprili 6, 2022, kutoka https://www.politico.eu/article/russia-expand-laws-criminalize-fake-news/.

39 Business Insider (2022). *A Russian court has declared Meta guilty of extremist activity but will still allow access to WhatsApp*. Imerejeshwa Machi 31, 2022, kutoka https://africa.businessinsider.com/tech-insider/a-russian-court-has-declared-meta-guilty-of-extremist-activity-but-will-still-allow/gbzm3dv; Access Now (@accessnow) Twitter post. 6:18 p.m. Machi 21, 2022. Imerejeshwa from Machi 31, 2022 kutoka https://twitter.com/accessnow/status/1505972115509555207.

40 Access Now (2021). *Belarusian election tainted by internet shutdown and state-sponsored violence.* Imerejeshwa Februari 18, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/belarusian-election-tainted-by-internet-shutdown-and-state-sponsored-violence/.

41 The Conversation (2022). *3 reasons Belarus is helping Russia wage war against Ukraine.* Imerejeshwa Machi 14, 2022, kutoka https://theconversation.com/3-reasons-belarus-is-helping-russia-wage-war-against-ukraine-177984.

42 Freedom House (2021). *Belarus: Freedom on the Net 2021 Country Report.* Imerejeshwa Februari 18, 2022, kutoka https://freedomhouse.org/country/belarus/freedom-net/2021.

## Amerika ya Kusini na Karibiani

Kulingana na nyaraka zetu, Cuba ndiyo nchi pekee katika eneo hilo iliyokata ufikiaji wa mtandao mwaka 2021. Mamlaka ilijibu maandamano na madai ya mabadiliko ya serikali kwa kuzima mitandao na kuzuia majukwaa. Mnamo Julai, Wacuba walipofurika barabarani kudai upatikanaji wa chakula, maji, dawa, na chanjo za COVID-19, serikali iliweka kizuizi kamili cha ujumla. Hata baada ya kurejesha ufikiaji wa mitandao, mamlaka ilizuia WhatsApp, Telegram na Signal.[43] Wakati VPN zilikuwa zikitumiwa na raia kupata huduma zilizozuiwa, kampuni ya mawasiliano inayomilikiwa na serikali ya ETECSA pia ilizuia maneno "VPN" na "libertad" ("uhuru") kutumwa kwa SMS.[44] Huduma za VPN zimekuwa zikifanya kazi mara kwa mara katika kisiwa hicho tangu Oktoba 2020.[45] Kwa kuongezea, serikali ya Cuba imeripotiwa kuwa imekuwa ikibatilisha SIM kadi za watu mahususi.[46] Hii inawaacha walioathirika - hasa wanaharakati na waandishi wa habari - kutengwa kabisa, kwani ETECSA ndio mtoaji pekee wa mtandao wa Cuba.


Huenda pia kulikuwa na uzimaji wa mitandao nchini Paraguay mwaka 2021, ingawa hatuna ushahidi wa kutosha wa kujumuisha usumbufu katika hifadhidata yetu ya STOP. Kulingana na utafiti wa teknolojia na shirika la jamii TEDIC, kuzimwa kwa mitandao huku kumeripotiwa kunaweza kuwa kulitokana na uvamizi wa kijeshi wa eneo hilo, na "katika siku chache kabla ya uingiliaji kati wa Kikosi Kazi cha Pamoja, watumiaji wote katika eneo moja [waliachwa] bila huduma yoyote."[47]

## Mashariki ya Kati na Afrika ya Kaskazini

Mnamo mwaka 2021, tuliandika kumbukumbu za kuzimwa kwa mitandao kwa angalau mara **23** katika nchi **tisa** za Mashariki ya Kati na Afrika ya Kaskazini, mara **tano** zaidi ya mwaka 2020. Sudani na Irani kila moja zilizima mitandao mara **tano**, idadi kubwa zaidi ya kufungwa kwa mitandao katika eneo hilo. Usumbufu mwingi katika nchi zote mbili ulilenga kunyamazisha upinzani.[48] Kihistoria, mamlaka katika nchi zote mbili zimeweka kizuizi ili kuzima maandamano na kuficha dhuluma mbaya na ukiukwaji

**Maeneo na upeo wa kufungwa mitandao katika Amerika ya Kusini na Karibiani mwaka wa 2021** ▾

**Daraja la 1:** Iliathiri jiji moja, jimbo au kijiji
**Daraja la 2:** Iliathiri zaidi ya jiji moja, ndani ya jimbo moja, mkoa au eneo
**Daraja la 3:** Iliathiri sehemu katika majimbo zaidi ya moja, mkoa, au eneo.
**Lisojulikana** Haijulikani sehemu zilizoathirika hasa




43 Access Now (2021). *"¡Patria y vida!": Cuba cuts internet access to gag protesters.* Imerejeshwa Februari 22, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/patria-y-vida-cuba/.

44 Yucabyte (2021). *"Libertad" y "VPN" bloqueadas para el servicio SMS en Cuba.* Imerejeshwa Aprili 2, 2022, kutoka https://www.yucabyte.org/2021/07/15/libertad-y-vpn-bloqueadas/.

45 ADNCuba (2020). *"La Isla queda a oscuras": cubanos denuncian bloqueo de servicios VPN.* Imerejeshwa Aprili 2, 2022, kutoka https://adncuba.com/noticias-de-cuba/actualidad/la-isla-queda-oscuras-cubanos-denuncian-bloqueo-de-servicios-vpn.


46 Radio y Televisión Martí (2021). *ETECSA blocks Internet access to Tania Bruguera, fails to prevent her participation in a UN event.* Imerejeshwa Februari 22, 2022, kutoka https://www.radiotelevisionmarti.com/a/etecsa-bloquea-acceso-a-internet-a-tania-bruguera-no-logra-impedir-su-participaci%C3%B3n-en-evento-de-onu/289238.html.

47 TEDIC (2021). *Call for Inputs UN OHCHR report on shutdowns and connectivity initiatives.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.tedic.org/wp-content/uploads/2022/03/TEDIC_ContributionOHCHR.pdf.

48 Tazama makala haya, e.g., Access Now (2021). *Iran: Internet blackouts curb protests and conceal human rights violations in Sistan and Baluchistan.* Imerejeshwa Aprili 19, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/iran-blackout-2021-internet-shutdowns-sistan-baluchistan/.

mwingine wa haki za binadamu.[49] Watu katika Palestina na Yemeni waliathiriwa na kuzimwa kwa mitandao kwa sababu ya mashambulizi ya miundombinu ya mawasiliano ya simu na usumbufu ulioratibiwa na kuongezeka kwa shughuli za kijeshi, wakati serikali za Omani na Jordani zililenga majukwaa ya mawasiliano yanayoibuka ambayo watu walikuwa wakitumia kujieleza kwa uhuru zaidi. Katika baadhi ya matukio, mamlaka iliamuru kukatizwa kwa mitandao kimakusudi katika jaribio la kuwazuia wanafunzi kufanya udanganyifu kwenye mitihani, tabia mbaya na isiyo na uwiano ambayo kulingana na rekodi zetu imeenea tu katika Mashariki ya Kati na Afrika ya Kaskazini tangu mwaka 2016. Wanaodumisha tabia hii katika mwaka 2021 ni Algeria, Iraqi, Jordani, Sudani, na Syria.

**Maeneo na upeo wa kufungwa kwa mitandao katika Mashariki Ya Kati na Afrika Kaskazini mwaka wa 2021**




49 Access Now (2020). *#IAmTheSudanRevolution: There's a direct link between internet shutdowns and human rights violations in Sudan.* Imerejeshwa Aprili 17, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/iamthesudanrevolution-theres-a-direct-link-between-internet-shutdowns-and-human-rights-violations-in-sudan/; Access Now (2020). *Iran has built an internet for oppression. Here's why you should care.* Imerejeshwa Aprili 19, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/iran-internet-shutdowns/.

# II. Vichochezi vya kuzima kwa mtandao mnamo 2021

Kama miaka mitano ya data katika hifadhidata yetu ya STOP inavyoonyesha, serikali kote ulimwenguni hugeukia kuzima mitandao katika majaribio ya kudhibiti watu. Mara nyingi tunaona usumbufu wa mitandao wakati wa maandamano, machafuko ya kijamii au kisiasa, uchaguzi na migogoro ya silaha. Data za mwaka 2021 inasimulia hadithi sawa. Mamlaka zilikata au kupunguza kasi ya kufikia mitandao, kufunga mifumo ya mawasiliano, au kuingilia mawasiliano ya mtandaoni wakati wa mvutano mkali, mara nyingi kama njia ya kudai au kudumisha mamlaka. Hiyo ni pamoja na kuzima mtandao wakati wa mapinduzi ya kijeshi.

**Sababu rasmi zilizotolewa kuunga mkono kufungwa kwa mtandao ulimwengu mzima zikilinganishwa na sababu halisi za kufanya hivyo mwaka wa 2021 ▾**

*Sehemu kubwa ya madai yaliyodaiwa kuwa ni ya kizalendo, yaliyoshuhudiwa wakati wa ukosefu wa utulivu wa kisiasa, ulitokea nyakati za kufungwa kwa mtandao nchini India.*




Katika siku ya kwanza ya mwaka, mamlaka ya India ilikata ufikiaji wa mitandao katika wilaya ya Jammu na Kashmir, mahali ambapo tunaona kuzimwa kwa mitandao zaidi kuliko mahali pengine popote duniani mnamo mwaka 2021. Baadaye katika mwezi huo, India ingeweka kizuizi cha ziada ili kuzima maandamano yaliyohusiana na Siku ya kusherehekea Jamhuri ya India.[50] Lakini mnamo Januari 1, tayari kulikuwa na vizuizi vinavyoendelea, sio India tu bali pia Ethiopia na Myanmar - ambayo kila moja ingeona kuzimwa mitandao zaidi katika miezi iliyofuata, katika muktadha wa hofu, vurugu na migogoro.

Mamlaka za serikali zinapowaingiza raia gizani wakati wa misukosuko, maisha yako hatarini. Kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kuzimwa kwa mitandao na ukiukaji wa haki za binadamu kote ulimwenguni.[51] Kuzimwa kwa mitandao kunakuza utamaduni wa kutoadhibiwa kwa uhalifu unaotendwa dhidi ya watu na kuweka ulimwengu mzima katika giza kuhusiana na ukubwa na ukali wa hali hiyo. Wanafanya iwe vigumu kwa waandishi wa habari na watetezi wa haki za binadamu kufikia maeneo yaliyoathirika ili kuripoti matukio na kuwajibisha serikali kwa ukatili.[52]

Kama tunavyooshesha hapa chini, kuzima mitandao daima ni hatari na hakuna tija, lakini huwa hivyo hasa wakati wa maandamano, machafuko ya kisiasa, vurugu za jumuia na vita. Kwa kuongeza, wanaweza kuwezesha uchochezi zaidi.

**Tarakimu ya mwaka wa 2021 ya sababu halisi za kufungwa kwa mtandao**




50 Access Now (2021). *Government orders internet shutdowns on India's Republic Day.* Imerejeshwa Machi 23, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/internet-shutdown-in-delhi-on-indias-republic-day/.

51 OHCHR (2021). *UN Human Rights Office Press briefing: Online.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://www.ohchr.org/sites/default/files/Documents/Press/Press%20briefing_140721.pdf.

52 Committee to Protect Journalists (2021). *Journalists struggle to work amid extended internet shutdowns in Myanmar, Ethiopia, Kashmir.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://cpj.org/2021/05/journalists-shutdowns-myanmar-ethiopia-kashmir.

## 2.1 Kuzimwa kwa mitandao wakati wa maandamano, misukosuko ya kisiasa na mapinduzi

Mamlaka nchini Bangladesh, Burkina Faso, Chadi, Cuba, Eswatini, India, Indonesia, Irani, Iraqi, Jordani, Kazakhstani, Myanmar, Pakistani, Senegal, Sudan ya Kusini, Sudani, Turkmenistani na Uganda zilitatiza au kukata kabisa muunganisho wa mawasiliano wakati wa maandamano mwaka 2021. Kama tulivyoona katika ripoti zilizopita,[53] serikali hutumia usumbufu wa mitandao kama chombo sio tu kuzuia na kufifisha uvunjaji wa haki za binadamu unaohusishwa na ukandamizaji wa vikosi vya usalama dhidi ya waandamanaji, haswa katika nchi ambazo zia utawala za kimabavu au demokrasia dhaifu.

### Mapinduzi ya Myanmar

Mnamo Februari 1, 2021, wakati jeshi lilipochukua udhibiti wa serikali, kulikuwa na ripoti nyingi za kuzimwa kwa mitandao kote Myanmar.[54] Kuzimwa kwa mitandao kuliathiri muunganisho wa intaneti na sauti katika majimbo kadhaa na kubadilika na kuwa usumbufu wa mtindo wa kutotoka nje, huku mamlaka ikikata ufikiaji wa mitandao kila siku kati ya Februari 15 na Aprili 28 wakati ufikiaji wa mitandao uliporejeshwa kwa kiasi.[55] Chini ya kifuniko cha kuzima mitandao, jeshi lilizidisha ghasia dhidi ya watu wanaopinga mapinduzi - ikiwa ni pamoja na kutumia risasi halisi, risasi za mpira na gesi ya machozi dhidi ya waandamanaji.[56] Mnamo Machi 3, wakati wa kukatika kwa umeme nchini kote, waandamanaji wasiopungua 38 waliuawa katika kile ujumbe wa Umoja wa Mataifa nchini Myanmar ulitangaza kuwa ni **"siku ya umwagaji damu mbaya zaidi tangu mapinduzi."**[57]

### Mapinduzi ya Sudani

Mamlaka ya Sudani ilifunga intaneti kwa nyakati tano tofauti mwaka wa 2021. Mnamo Oktoba 25, jeshi liliweka vikwazo vya mitandao wakati walipon-yakua mamlaka kutoka kwa serikali ya mpito katika mapinduzi ya kijeshi.[58] Waliwazuilia kiholela maafisa kadhaa wa serikali, akiwemo waziri mkuu. Wakati watu wa Sudani walipoingia mitaani kukemea vitendo vya jeshi, walikabiliwa na usumbufu wa ziada wa mitandao na vurugu na vikosi vya kijeshi, ambavyo

> **Serikali ilikata mawasiliano ya mitandao baada ya jeshi kuwageuka washirika wao katika uongozi wa mpito, serikali ya kiraia. Mamilioni ya watu waliandamana na wakakumbana na dhoruba za vurugu na ghasia pamoja na hujuma. Vifaru, magari ya polisi, yalitumika dhidi ya uasi wa raia. Majeshi yalikabiliana na raia kama ambao walikuwa vitani, wakirusha risasi amazo ziliua mashahidi wengi. Niliponea chupuchupu badala ya risasi kunikosa na kumuingiakijana nyuma yangu, na akafariki. Maisha ni magumu bila ya intaneti.**



Photo credit: Bertramz

Bibi mmoja mwandishi wa habari za kibinafsi alikwenda maandamanoni baada ya mapenduzi ya kijeshi ya Oktoba 2021, huko Sudani. Kwa kujawa na kiwewe kwa unyama uliotekelezwa na wanajeshi, alivunjika moyo zaidi alipokosa matumizi ya mitandao ambayo huitumia kupata habari.

25 Novemba, 2021
Omdurman, Sudani

53 Access Now (2019). *Targeted, cut off, and left in the dark: The #KeepItOn report on internet shutdowns in 2019.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/cms/assets/uploads/2020/02/KeepItOn-2019-report-1.pdf.

54 BBC News (2021). *Myanmar coup: Aung San Suu Kyi detained as military seizes control.* Imerejeshwa Februari 23, 2022, kutoka https://www.bbc.com/news/world-asia-55882489.

55 KrASIA (2021). *Myanmar's mobile internet unblocks online banking, possible national intranet prompts concerns.* Imerejeshwa Februari 18, 2022, kutoka https://kr-asia.com/myanmars-mobile-internet-unblocks-online-banking-possible-national-intranet-prompts-concerns.

56 Al Jazeera (2021). *Myanmar police used machine guns against protesters, says Amnesty.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://www.aljazeera.com/news/2021/2/11/myanmar-police-deployed-machine-guns-against-protesters

57 Nikkei Asia (2021). *Myanmar coup, from Feb. 20 to March 18: UN team urges whistleblowers to report illegal orders.* Imerejeshwa Machi 22, 2022, kutoka https://asia.nikkei.com/Spotlight/Myanmar-Crisis/Myanmar-coup-from-Feb.-20-to-March-18-UN-team-urges-whistleblowers-to-report-illegal-orders.

58 Access Now (2021). *Authorities in Sudan must stop imposing telecommunication blackouts to control information flow during military coup.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/sudan-internet-shutdown-military-coup/.

vilisababisha mauaji ya watu saba na wengine 140 kujeruhiwa.[59] Mamlaka pia zilipunguza ufikiaji wa mitandao wakati wa mitihani ya shule.

Kama Myanmar, Sudani ina historia ya giza ya kuendeleza ufungaji wa mitandao unaosababisha ukiukaji wa haki za binadamu. Baada ya kuondolewa madarakani kwa utawala wa Omar Al-Bashir mnamo Aprili 2019, jeshi lilifanya ukatili dhidi ya watu wa Sudani, pamoja na mauaji ya raia 100 na kujeruhi wengine wengi[60] na ubakaji wa wanawake 70[61] katika kiwingu cheusi cha kuzima kabisa kwa mitandao mwezi Juni 2019.

## Ukandamizaji mbaya wa Irani dhidi ya maandamano

Nchini Irani, mamlaka zilijibu maandamano kwa kukata upatikanaji wa mitandao ya simu kuanzia Februari 24-28 huko Sistan na Baluchistani, ambapo zaidi ya 95.7% ya watu hutegemea mitandao ya simu ili kuendelea kuwasiliana.[62] Waliripoti kuzima ufikiaji wa mitandao ili kuficha ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu na uhalifu wa kimataifa unaowezekana, kama vile mauaji ya kiholela. Kwa mujibu wa vyombo vya habari, Jeshi la Walinzi wa Mapinduzi ya Kiislamu, tawi la jeshi la Irani liliwafyatulia risasi raia wachuuzi wa mafuta ambao hawakuwa na silaha na kuwauwa watu 10 akiwemo mtoto.[63]

Hizi si mbinu mpya kwa mamlaka ya Irani. Mnamo mwaka 2019, Amnesty International ilithibitisha vifo vya watu 304 waliouawa na watu wa usalama wa Irani wakati wa kuzimwa kwa mitandao kwa wiki moja kwa lengo la kukatisha maandamano. Zaidi ya vifo 220 kati ya hivyo vilifanyika ndani ya saa 48 baada ya mitandao kuzimwa.[64]

## Nchi nyingine zilizo kwenye uangalizi

Nchi nyengine kadhaa ambazo zilikabiliana na maandamano kwa kulazimisha kuzimwa kwa mtandao mnamo mwaka 2021 ni pamoja na:

**Jordani:** Mnamo Machi 2021, maandamano yalizuka baada ya wagonjwa saba wa COVID-19 kufa kwa sababu ya ukosefu wa usambazaji wa oksijeni katika hospitali ya Al-Salt. Kwa hivyo uongozi huko Jordani ulisitisha huduma za utiririshaji habari wa moja kwa moja za Facebook ili kuzuia watu kushiriki video, pamoja na zile zinazoandika polisi kuwakandamiza waandamanaji[65] - mbinu ya udhibiti ambayo serikali imetumia mara kwa mara tangu mwaka 2018.

**Pakistani:** Mnamo Aprili 16, baada ya wiki kadhaa za maandamano ya kupinga Ufaransa kuhusu vibonzo vilivyochapishwa na jarida la kejeli la Ufaransa la Charlie Hebdo, Wizara ya Mambo ya Ndani iliamuru Mamlaka ya Mawasiliano ya Pakistani kuzuia Twitter, Facebook, WhatsApp, YouTube na Telegram.[66] Ili serikali iimarishe zaidi udhibiti wake wa anga za kidijitali nchini, Wizara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya Pakistani ilianzisha kanuni kali[67] mnamo Oktoba 2021. Kanuni hizi huwezesha mamlaka kudhibiti na kuhakiki maudhui yanayochapishwa kwenye mitandao ya kijamii kadri wanavyoona inafaa, kielelezo cha hatari kinachozuia watu kufurahia haki za kimsingi.[68]

**Eswatini:** Mamlaka zilijibu maandamano ya kuunga

59 Reuters (2021). *Seven killed, 140 hurt in protests against Sudan military coup.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://www.reuters.com/world/africa/military-forces-arrest-senior-civilian-figures-sudan-al-hadath-tv-2021-10-25/.

60 The New York Times (2019). *100 Killed in Sudan and Dozens of Bodies Are Pulled From Nile, Opposition Says.* Imerejeshwa Machi 23, 2022, kutoka https://www.nytimes.com/2019/06/04/world/africa/sudan-war-facts-history.html.

61 The Guardian (2019). *Sudanese doctors say dozens of people raped during sit-in attack.* Imerejeshwa Februari 14, 2020, kutoka https://www.theguardian.com/world/2019/jun/11/sudan-troops-protesters-attack-sit-inrape-khartoum-doctors-report.

62 Communication Regulatory Authority (2021). *ICT Development in Sistan and Baluchestan Province - Volume: Azar 99.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://mis.ito.gov.ir/ictindex/viewprovinceindex/15.

63 *Tazama maelezo ya supra* 48.

64 Amnesty International (2021). *Iran: A Web of Impunity: The Killings Iran's Internet Shutdown Hid.* Imerejeshwa Februari 18, 2022, https://www.amnesty.org/en/documents/mde13/3308/2020/en/.

65 Access Now (2021). *Jordan's internet throttling to censor protesters must end.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/jordan-protest-throttling/.

66 France 24 (2021). *Pakistan orders temporary social media shutdown after violent protests.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://www.france24.com/en/live-news/20210416-pakistan-orders-temporary-social-media-shutdown-after-violent-protests.

67 Scribd.com (2021). *Revised Rules, 2021 (12.10.2021 after Approval of the Cabinet).* Imerejeshwa Machi 23, 2022, kutoka https://www.scribd.com/document/532380328/Revised-Rules-2021-12-10-2021after-Approval-of-the-Cabinet.

68 RSF (2021). *Another attempt by Pakistan's government to censor social media.* Imerejeshwa Machi 23, 2022, kutoka https://rsf.org/en/news/another-attempt-pakistans-government-censor-social-media.

mkono demokrasia kwa kukata ufikiaji wa mtandao kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 2021, Juni 29 na Oktoba 15. Walitaja hitaji la kudhibiti "machafuko na vurugu."[69]

**Cuba:** Kama tunavyoona hapo juu, mamlaka ya Cuba ilijibu maandamano na wito ulioenea wa mageuzi ya serikali mnamo Julai 2021 kwa kuzuia ufikiaji wa mitandao na majukwaa ya mawasiliano.[70] Hii ni pamoja na kufanya mitandao ya simu karibu kutofanya kazi.


**Burkina Faso:** Mnamo Novemba 20, 2021, mamlaka nchini Burkina Faso ilifunga intaneti ya simu kwa takriban siku tisa kwa minajili ya kupambana na maandamano wakitaja sababu zisizo wazi za "usalama wa umma" na "ulinzi wa taifa".[71] Hii ilikuwa mara ya kwanza kukata ufikiaji wa mitandao kulingana na hifadhidata yetu ya STOP, lakini kufikia Januari 23, 2022, serikali ya Kaboré ilikuwa imefunga intaneti kwa matukio matatu tofauti.

## 2.2 Kuzimwa kwa mitandao wakati wa uchaguzi

Kuzimwa kwa mtandao wakati wa uchaguzi ni janga kwa demokrasia. Hata hivyo katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, mamlaka za serikali zimeendelea kulazimisha kufungwa kwa mitandao, kabla ya, wakati wa, au mara tu baada ya uchaguzi. Mnamo mwaka 2021, muungano wa #KeepItOn ulirekodi kufungwa kwa mitandao mara **saba** kuhusiana na uchaguzi katika nchi **sita**: Chadi, Jamhuri ya Kongo, Irani, Niger, Uganda na Zambia.[72] Hii ni chini ya rekodi yetu ya mwaka 2020 ya kufungwa kwa mitandao katika chaguzi **10** katika nchi **saba**, rekodi yetu ya mwaka 2019 yenye matukio **12** ya kuzimwa kwa mitandao katika nchi **saba**, na rekodi yetu ya 2018 yenye matukio **12** katika nchi **saba**.

Kati ya matukio haya 4 ya kufungwa kwa mitandao yalifanyika katika nchi za Kiafrika, ambapo kusimamishwa kwa uchaguzi bado ni jambo la kawaida licha ya kuongezeka kwa upinzani na kurudi nyuma kwa sheria. Yafuatayo ni maelezo juu ya usumbufu, kwa mpangilio wa matukio.

**Idadi ya kufungwa kwa mitandao kwa ajili ya ghasia za uchaguzi**




**Uganda**, mhusika wa mara kwa mara wa kuzima intaneti katika uchaguzi, ilizuia ufikiaji wa majukwaa na zana za mawasiliano ya kidijitali na kisha kuzima mtandao kabla ya uchaguzi wake wa Januari 2021. Mamlaka ilianza kwa kusukuma na kuzuia maombi ikiwa ni pamoja na Facebook, Twitter, WhatsApp na Instagram, pamoja na iOS App Store na Google Play Store. Pia walizuia ufikiaji wa VPN. Tume ya Mawasiliano ya Uganda kisha iliamuru watoa huduma za mtandao kupunguza ufikiaji nchini kote.[73] Kusitishwa huko kuliwaweka Waganda gizani kwa siku tano na hivyo kufanya iwe vigumu sana kwa raia kuendelea na maisha yao ya kila siku, kupata taarifa kuhusu matokeo ya uchaguzi au kushiriki kwa uhuru katika mazungumzo ya kidemokrasia.[74] Tangu wakati huo, mamlaka ya Uganda imekataa kuifungia Facebook[75] ili kulipiza kisasi kwa kampuni hiyo kuondolewa kwa akaunti za maafisa wa serika-

69 Access Now (2021). *#KeepItOn: Eswatini authorities shut down internet to quell protests, ask people to email grievances.* Imerejeshwa Machi 21, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/keepiton-eswatini-protests/.

70 *Angalia supra noti ya* 43.

71 Access Now (@accessnow). Post ya Twitter saa 6:38 mchana. Novemba 23, 2021. Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://twitter.com/accessnow/status/1463124812084260868

72 *Angalia supra* noti ya 10

73 Quartz (2021). *Uganda has shut down all social media two days ahead of a tense election.* Imerejeshwa Machi 21, 2022, kutoka https://qz.com/africa/1956188/uganda-shuts-social-media-ahead-of-election-army-out-in-streets/; Access Now (2021). *"No matter what they do, the world is watching": Some Ugandans are back online after internet shutdown during presidential election.* Imerejeshwa Machi 16, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/the-world-is-watching-uganda-elections/.

74 *Angalia supra* noti 9.

75 Paradigm Initiative (2021). *Continued Facebook Shut-down Inconveniencing Ugandans.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://paradigmhq.org/continued-facebook-shut-down-inconveniencing-ugandans/.



Habari kamili imechapishwa katika NTV Uganda 18 Januari 2021.
Photo credit: Direct Relief

**Mohammed ni mtetezi wa haki za wasiojiweza. Anategemea intaneti/mitandao kwa ajili ya kutekeleza kazi zake za kila siku. Kufungwa ghafla kwa mitandao nchini Uganda, mbali na kumdhiki kinafsi, pia alitambua jinsi yeye na jamii yake ilivyokuwa inatengwa na kutatizwa kuishi maisha yao ya kawaida, kwa kunyang'anywa fursa za kusoma na kupata kazi za mitandaoni wakati huo wa rabsha.**

**Januari 13, 2021**
**Mohammed Kimbugwe**
**kutoka Uganda**

**#KeepItOn**

**Uganda ina takriban 12.4% ya watu wanaoishi na ulemvu na wanajikakamua kimaisha kupambana na hali ngumu za kimaisha kama mfumko wa bei wa vyombo vya mawasiliano na teknolojia, na paingiapo kufungwa kwa mitandao, maumivu hayo huwa maradufu ya hali yake ya kawaida. Walemavu hupata pigo mara mbili mitandao inapofungwa, pigo la ulemavu na ukosefu wa mawasiliano ya kidijitali. Pale tulipodhani kuwa mitandao imetufungulia fursa kabambe za kuboresha maisha, ambazo tulinyimwa zamani, kufungwa kwa mitandao kunatukumbusha kuwa safari bado ingali ndefu ya kujumuishwa maishani.**

Ii wanaotuhumiwa kutaka kudanganya mjadala wa umma kabla ya uchaguzi[76] wa Januari 2021. Usumbufu huo ulikuwa mkubwa na wa kina zaidi kuliko kufungwa hapo awali mnamo mwaka 2016, wakati mamlaka ya Uganda ilizuia pesa za simu na mitandao ya kijamii mara mbili - wakati wa uchaguzi na sherehe za kuapishwa kwa Rais Yoweri Museveni [77]ambaye ameng'ang'ania madarakani tangu 1986.

Nchini **Niger**, serikali ilijibu maandamano yaliyozuka baada ya uchaguzi wa Februari 21 kwa kuzima mitandao ya simu kote nchini kuanzia Februari 24.[78] Mamlaka haikurejesha ufikiaji kamili wa mitandao kwa siku 10 na maafisa wa serikali hawakutoa maelezo kwa usumbufu mkubwa.

**Jamhuri ya Kongo** ilifuata mkondo huo mnamo Machi 21, wakati serikali ilitekeleza kuzima kabisa kwa mitandao saa chache kabla ya upigaji kura kuanza. Kuzimwa kwa mitandao kumekata miunganisho ya mawasiliano na intaneti ya simu, pamoja na kuzuia ujumbe wa SMS na ilidumu hadi Machi 23.[79] Tabia za zamani hazipotei. Mnamo mwaka 2016, Waziri wa Mambo ya Ndani Raymond Mboulou alikuwa ameamuru kampuni za mawasiliano kuzima huduma za simu, intaneti na SMS kwa saa 48 wakati wa uchaguzi wa rais kwa "sababu za ulinzi na usalama wa taifa."[80]

Mnamo tarehe 20 Juni, mamlaka nchini **Irani** ilijibu makabiliano kati ya makabila mawili ya ndani kufuatia uchaguzi wa mabaraza ya mitaa kwa kukata mawasiliano ya simu kwa siku nzima huko Yasuj, mji mkuu wa mkoa wa Kohgiluyeh na Mkoa wa Boyer-Ahmad.[81] Kwa bahati nzuri, hakukuwa na

76 Committee to Protect Journalists (2016). *Uganda blocks social media and mobile phone services during voting.* Imerejeshwa Aprili 7, 2022, kutoka https://cpj.org/2016/02/uganda-blocks-social-media-and-mobile-phone-servic/.

77 Global Voices Advox (2016). *Social media blocked in Uganda ahead of President Museveni's inauguration.* Imerejeshwa Aprili 7, 2022, kutoka https://advox.globalvoices.org/2016/05/11/social-media-blocked-in-uganda-ahead-of-president-musevenis-inauguration/.

78 Business Insider (2021). *#WhatsHappeningInNiger: The internet shutdown in Niamey threatens Niger's democracy and its people's right to free speech.* Imerejelewa Machi 24, 2022, kutoka https://africa.businessinsider.com/local/leaders/whatshappeninginniger-the-internet-shutdown-in-niamey-threatens-nigers-democracy-and/p7l4nhk.

79 AfricaNews (2021). *Congo Election: Low voter turn out, internet shutdown, mark polls.* Imerejeshwa Machi 23, 2022, kutoka https://www.africanews.com/2021/03/21/congo-election-low-voter-turn-out-internet-shutdown-mark-polls/.

80 Al Jazeera (2016). *Congo holds presidential elections under media blackout.* Imerejeshwa Machi 23, 2022, kutoka https://www.aljazeera.com/news/2016/3/20/congo-in-media-blackout-for-presidential-elections.

81 Filterwatch (2021). *Internet Shutdown Trends in Iran: November 2019 to July 2021.* Imerejeshwa Aprili 6, 2022, kutoka https://filter.watch/en/2021/09/03/internet-shutdown-trends-in-iran-from-november-2019-to-july-2021/.

kuzimwa kwa mitandao wakati wa uchaguzi mkuu ambao ulifanyika siku chache mapema Juni 18.

Access Now, washirika wetu wa kikanda na wanachama wengine wa muungano wa kimataifa wa #KeepItOn walifanikisha kutofungwa kwa mitandao nchini **Zambia** wakati wa uchaguzi wa Agosti 12, wakitoa wito kwa serikali kudumisha mtandao wazi na unaoweza kufikiwa.[82] Licha ya mamlaka ya Zambia kutoa taarifa kwa umma kukanusha[83] vikali uvumi kwamba ilikuwa inapanga kuzima mtandao siku ya uchaguzi, ilifanya hivyo.

Mamlaka zilizuia ufikiaji wa majukwaa ya mitandao ya kijamii ikiwa ni pamoja na WhatsApp, Facebook, Twitter na Instagram.[84] Chapter One Foundation (Ltd) iliwasilisha haraka kesi ya kupinga usumbufu[85] huo na siku mbili baadaye Mahakama Kuu ya Zambia iliamuru serikali kurejesha ufikiaji wa mitandao mara moja.[86] Ingawa kuzimwa kwa mitandao hakukupaswa kuamriwa hivyo, kwa vile kusitishwa kwa shughuli hizo zote kunaharibu uchaguzi, uamuzi huo ni ushindi muhimu dhidi ya aina hii ya shambulio la kudhuru haki kwa demokrasia. Kwa hakika, kama tunavyoangazia katika sehemu ya 4.2 hapa chini, mashirika ya kiraia katika baadhi ya nchi za Afrika yalipambana na kuzimwa kwa mtandao katika mahakama za sheria mwaka 2021, mchango muhimu sana katika vita dhidi ya kuzimwa kwa mtandao duniani kote.

Hatimaye, kama tulivyoona hapo awali, **serikali ya Urusi** ilifanya jitihada kubwa kuwanyima wapiga kura idhini ya kufikia programu ya Smart Voting ya kiongozi wa upinzani Alexey Navalny, ambayo iliwaruhusu wapiga kura kufuatilia kwa karibu na kupokea masasisho kuhusu uchaguzi wa Septemba. Mnamo Septemba 2, mamlaka ya Urusi iliamuru Apple na Google kuondoa programu kutoka kwenye maduka yao ya programu na majukwaa.[87] Baadaye ilijulikana kwamba mawakala wa serikali ya Urusi walitishia wafanyakazi wa kampuni hizi.[88] Makampuni yote mawili hatimaye yalikubali shinikizo na wakaondoa programu kwenye maduka yao. Wakati huo huo, juhudi za serikali yenyewe za kuzuia ufikiaji wa programu zilisababisha kuzuiwa kwa muda kwa huduma za Google na Cloudflare DNS, VPN, Hati za Google na video za YouTube zinazotumiwa na mradi wa Smart Voting na kuzimwa kwa gumzo la Smart Voting kwenye Telegram.

**Jinsi muungano wa #KeepItOn unavyoitikia**

Inasikitisha kuona serikali yoyote ikitenganisha watu wake wakati wa uchaguzi, ikishambulia haki za binadamu na kudhoofisha uadilifu wa uchaguzi. Hata hivyo, katika miaka ya hivi majuzi, muungano wa #KeepItOn umeongezeka na kuimarisha utetezi wake kuhusu kusitishwa kwa shughuli za uchaguzi, tumerekodi kushuka kwa kasi kwa utekelezaji huu. Hasa, kulikuwa na nchi kadhaa ambazo hapo awali zilikata ufikiaji wa mitandao wakati wa

82 Access Now (2021). *As a contentious election nears, rights groups urge Zambia to #KeepItOn.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/as-contentious-election-nears-rights-groups-urge-zambia-to-keepiton/.

83 LusakaTimes.com (2021). *There will be No Internet Shutdown in Zambia, Blackout Information is False and Calculated to Cause Alarm.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.lusakatimes.com/2021/08/07/there-will-be-no-internet-shutdown-in-zambia-information-is-false-and-calculated-to-cause-alarm/.

84 CNN (2021). *Social media and messaging apps appear to be shutdown in Zambia on election day, Facebook says.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://edition.cnn.com/2021/08/12/africa/zambia-election-social-media-blackout-intl/index.html.

85 Daily Nation (2021). *ZICTA sued over internet shutdown.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://dailynationzambia.com/2021/08/zicta-sued-over-internet-shutdown/.

86 NewZimbabwe.com (2021). *Zambia's High Court Orders Restoration Of Internet Services.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.newzimbabwe.com/zambias-high-court-orders-restoration-of-internet-services/.

87 Access now (2021). *Not good enough: Apple, Google bow to government pressure, censor content during Russian elections.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka
https://www.accessnow.org/apple-google-censor-russian-elections/

88 The Washington Post (2021). *Analysis | The Kremlin forced U.S. tech firms to shut down an app some Russian voters hoped to use. Now what?* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://www.washingtonpost.com/politics/2021/09/30/kremlin-forced-us-tech-firms-shut-down-an-app-its-opponents-were-using-now-what/

uchaguzi ambazo hazikubadilisha swichi ya kuua ufikiaji mitandao mnamo 2021, ikijumuisha Benin,[89] Iraqi na Gambia. Kwa mwaka mzima, huku Access Now ikiendelea kutayarisha mpango wetu wa Kutazama Uchaguzi, tulifanya kazi na wanachama wa muungano wa #KeepItOn duniani kote ili kushirikisha serikali, makampuni na washika dau wengine katika vita vya kukomesha kuzimwa kwa mitandao wakati wa uchaguzi.[90] Hii ilimaanisha kuwa katika nchi ambazo serikali ziliweka vikwazo, umoja huo mara nyingi uliweza kutumia warsha za kujengea uwezo[91] na mbinu nyinginezo[92] ili kuyapa makundi ya asasi za kiraia pamoja na watu binafsi rasilimali za kujiandaa na kukwepa uzuiaji pamoja na kuweka kumbukumbu za kuzimwa mtandao na ushawishi wa kisheria[93] na utetezi katika mikutano ya kitaifa na kimataifa.

## 2.3 Kuzimwa kwa mitandao katika maeneo ya migogoro

Duniani kote, pande zinazopigana zimezidisha mashambulizi dhidi ya huduma muhimu za kiraia wakati wa vita na vurugu, ikiwa ni pamoja na mashambulizi yanayolenga miundombinu ya mawasiliano ya simu. Kuzimwa kwa mitandao wakati wa migogoro huweka maisha katika hatari na kuwanyima watu ufikiaji wa taarifa zinazookoa maisha, ndani na nje ya maeneo yenye migogoro. Vyama vya nje haviwezi kuelewa kile kinachotokea chinichini, na kukwamisha juhudi za kimataifa za kibinadamu na kuzuia uwekaji kumbukumbu wa uhalifu wa kivita na ukatili unaofanywa dhidi ya raia. Mbaya zaidi, kuzimwa kwa intaneti kunakofanywa kupitia uharibifu wa kimakusudi wa mitandao na mifumo ya mawasiliano ya simu na miundo mbinu kunaweza kuacha watu walioathiriwa kutengwa na ulimwengu kwa miezi kadhaa, na kuwafanya watu wahangaike na ukarabati ambao unaweza kuathiriwa na kuzimwa kwa mitandao siku zijazo.

Mnamo mwaka 2021, tuliona mwendelezo wa kuzimwa kwa mitandao eneo la Tigray nchini Ethiopia, ambayo ilianza Novemba 2020 na inaendelea hadi leo, katika muktadha wa vita vya wenyewe kwa wenyewe vinavyoendelea, uhalifu dhidi ya binadamu na utakaso wa kikabila.[94] Uzimaji wa mtandao huo uliathiri mikoa jirani ya Amhara na Afar kufuatia kuenea kwa mzozo katika maeneo hayo. Pia tuliandika kumbukumbu za kuzimwa kwa mitandao katika maeneo yenye mizozo katika Ukanda wa Gaza, wakati jeshi la Israeli lilipokuwa likijihusisha na mashambulizi ya mabomu katika mzozo unaoendelea na Wapalestina kuhusu kukalia kwa mabavu Palestina, na Myanmar, ambapo jeshi liliteka na kupigana ili kudumisha udhibiti. Huko Afghanistani, wapiganaji wa Talibani waliposonga mbele kuelekea kuimarisha udhibiti wa nchi hiyo kufuatia kujiondoa kwa jeshi la Marekani, walizuia mawasiliano katika mkoa wa Panjshir ambapo viongozi wa upinzani walikuwepo na ambapo watu walikuwa wakikabiliwa na uhaba mkubwa wa chakula, maji, dawa na mahitaji mengine ya kimsingi.[95] Data iliyokusanywa kupitia mradi wetu wa STOP juu ya kuzimwa kwa mitandao nchini Azabajani, Syria na Yemeni[96] katika kipindi cha miaka mitano iliyopita inaonyesha muundo: **miundombinu ya mtandao inalengwa na wanajeshi wakati wa migogoro inayoendelea**.

89 Internet Society (2021). *Keeping the Internet on during Benin's Presidential Elections.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://www.internetsociety.org/blog/2021/06/keeping-the-internet-on-during-benins-presidential-elections/.

90 *Angalia supra* noti ya 10.

91 YouTube video (2021). *[WEBINAR] #KeepItOn during a shutdown: how to measure, document, and circumvent internet shutdowns.* Imerejeshwa Februari 18, 2022, kutoka https://www.youtube.com/watch?v=aFlBrRXKm2E.

92 Access Now (2021). *Internet shutdowns and elections handbook.* Imerejeshwa Februari 18, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/internet-shutdowns-and-elections-handbook/.

93 Paradigm Initiative (2021). *5 NGOs, 4 Journalists Sue Federal Government at ECOWAS Court Over Twitter Ban.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://paradigmhq.org/5-ngos-4-journalists-sue-federal-government-at-ecowas-court-over-twitter-ban/.

94 Amnesty International (2021). *Crimes Against Humanity in Ethiopia's Western Tigray Zone.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://www.amnesty.org/en/latest/news/2022/04/ethiopia-crimes-against-humanity-in-western-tigray-zone/.

95 *Angalia Supra* noti ya 21.

96 Access Now (2020). *#KeepItOn: As Yemen's war goes online, internet shutdowns and censorship are hurting Yemenis.* Imerejeshwa Machi 23, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/keepiton-as-yemens-war-goes-online-internet-shutdowns-and-censorship-are-hurting-yemenis/

## Ethiopia: Kukatika kwa intaneti huko Tigray kunaongeza athari za vita vya kikatili vya wenyewe kwa wenyewe

Baada ya mzozo kuzuka kati ya Vikosi vya Ulinzi vya Ethiopia na vikosi vya eneo huko Tigray, tuliona mfululizo wa kukatika kwa mitandao na kuathiri watu katika eneo hilo, kuanzia Novemba 2020 mpaka 2021 hadi leo. Ufikiaji wa mitandao umerejeshwa katika mikoa jirani ya Afar na Amhara ambayo iliathiriwa na mzozo huo na tuliona kuzimwa kwa mitandao mnamo 2021.[97]

> **Kutikiswa mara kwa mara kwa mitandao, kwasababisha athari mbaya kwa watu wa Tigray kwa kuzifinya habari kuhusu yanayotendeka maishani mwao. Si hili tu, bali pia linazidisha janga la kiuchumi kwa watu wa Tigray.**



Photo credit: Peter Machacek

**Yosef, anafanya kazi ya huduma ya wateja huko Shire. Anaelezea vile kufungwa kwa mitandao ya kijamii kunaathiri uchumi wa eneo hilo na kukatisha tamaa na kuvurujua watu na jamii zao, na kufanya kazi vitongojini kuwa mbaya zaidi.**

**Aprili 20, 2021**
**Tigray, Ethiopia**

Ni vigumu kueleza madhara makubwa ya mzozo wa muda mrefu na kukatika kwa mawasiliano yanayoendelea kwa Waethiopia huko Tigray ambapo pande zinazopigana zimeongeza kasi ya kukatika kwa umeme na kutekeleza uhalifu wa kutisha dhidi ya binadamu.[98] Wafanyakazi wa kibinadamu na wanaotoa misaada hawawezi kufikia maeneo yenye migogoro na hawawezi kuwasiliana wao kwa wao ili kutoa huduma muhimu kama vile chakula, maji, nguo na dawa hivyo kuwaacha watu katika hatari ya magonjwa na njaa.[99] Umoja wa Mataifa ulikadiria kuwa takribani watu 350,000 walikuwa kwenye baa la njaa kati ya Mei na Juni 2021.[100] Watetezi wa haki za binadamu, waandishi wa habari na jumuia ya kimataifa wanajitahidi kuripoti kuhusu mzozo unaoendelea na mgogoro wa kibinadamu. Kufinywa kwa habari kulikoundwa na kuzimwa kwa mitandao pia kumeruhusu habari potofu kustawi na kuwaweka watu katika hatari kubwa zaidi.[101]

### Jinsi kuzimwa kwa mitandao kunavyozuia misaada

Mnamo mwaka wa 2021, Adele Khodr, mwakilishi wa UNICEF nchini Ethiopia alisisitiza haja ya dharura ya misaada kufikia sehemu za Tigray ambazo hazijafikiwa kwa miezi kadhaa.

“Tunajua tuna watoto 33,000 walio katika hatari kubwa ya magonjwa na vifo, wanakuwa wagonjwa sana na hatimaye kufariki. Tunahitaji kuwafikia watoto hao haraka iwezekanavyo,” alisema. "Ukosefu wa simu au mtandao, hata hivyo unaweza kutatiza juhudi zozote za usaidizi."

"Ikiwa hatuna vifaa vya mawasiliano ya simu, hatuwezi kutuma watu vijijini na kuhakikisha usalama wao. Ni rahisi sana," alisema.[102]

---

**97** Belay Manaye (@Belay_Ma) Twitter Post. 5:03 am. January 2, 2022. Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://twitter.com/Belay_Ma/status/1477505695117455361.

**98** Global Voices (2021). *Vicious mass rape of women has become a weapon against the Tigray in Ethiopian war.* Imerejeshwa Machi 22, 2022, https://globalvoices.org/2021/07/05/vicious-mass-rape-of-women-has-become-a-weapon-against-the-tigray-in-ethiopian-war/; BBC News (2021). *Evidence suggests Ethiopian military carried out massacre in Tigray.* Imerejeshwa Machi 22, 2022, kutoka https://www.bbc.com/news/world-africa-56603022

**99** The Guardian (2021). *Tigray ceasefire: aid workers demand telecoms be restored.* Imerejeshwa Machi 22, 2022, kutoka https://www.theguardian.com/global-development/2021/jul/02/tigray-ceasefire-aid-workers-demand-telecoms-be-restored.

**100** IPC Portal (2021). *Ethiopia: Famine Review Committee confirms very high levels of acute food insecurity and Risk of Famine in Tigray.* Imerejeshwa Machi 22, 2022, kutoka https://www.ipcinfo.org/ipcinfo-website/alerts-archive/issue-42/en/.

**101** Addis Zeybe (2021). *Does Social media intensify the conflict in Northern Ethiopia?* Imerejeshwa Machi 25, 2022, https://addiszeybe.com/featured/politics/currentaffairs/analysis/does-social-media-intensify-the-conflict-in-northern-ethiopia.

**102** *Angalia supra* noti ya 99.

## Matumizi ya Facebook kama silaha

Wakati watu wa Tigray walisalia gizani mwishoni mwa mwaka 2021, mzozo ulizidi ikiwa ni pamoja na mitandaoni ambapo majukwaa ya mitandao ya kijamii yalitumiwa kuchochea vurugu za kikabila na chuki dhidi ya makundi yaliyohusika katika mgogoro huo. Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed alitumia matamshi ya chuki kwenye Facebook katika juhudi za kuchochea ghasia dhidi ya waasi wa Tigray.[103] Ujumbe wa Ahmed ulipata mvuto miongoni mwa maafisa wa serikali ambao waliiga lugha yake aliporejelea mashambulizi dhidi ya Watigrayani.[104] Kuongezeka huku kulikuja pamoja na historia mbaya ya matamshi ya chuki mtandaoni ya viongozi wa ngazi za juu ndani ya serikali ya Ethiopia, makundi ya waasi wenye silaha ndani ya nchi hiyo na wafuasi wao kote ughaibuni.[105]

Miito hii hatari na yenye nguvu ya vurugu kwenye Facebook iliibua kilio cha umma na wito kutoka kwa wanaharakati kwa kampuni mama ya Facebook ya Meta kuboresha mbinu yake ya kudhibiti maudhui katika muktadha wa mivutano na migogoro nchini Ethiopia. Kushindwa kwa Meta kukandamiza au kujibu ipasavyo[106] hotuba iliyoelezewa kama mauaji ya halaiki inaonekana laana zaidi baada ya mtoa taarifa Frances Haugen kuvujisha nyaraka zinazoonyesha kwamba Meta ilijua jukwaa lake lilikuwa linatumiwa kuchochea vurugu lakini ilifanya juhudi kidogo sana kukomesha hilo.[107] Mnamo mwaka 2021, Meta ilichukua hatua ya kuchelewa kufuta baadhi ya maudhui yanayochochea vurugu.[108] Hata hivyo, ni wazi Meta na majukwaa mengine ya mtandaoni bado hayajashughulikia ipasavyo changamoto ya kuzuia utumiaji wa huduma zao kama silaha.

## Mashambulizi ya Israel kwenye Ukanda wa Gaza

Mnamo Mei 2021, vikosi vya jeshi la Israeli vilishambulia kwa mabomu na kuteketeza au kuharibu miundombinu ya mawasiliano na kusababisha kuzima kabisa kwa mitandao na kwa sehemu katika Ukanda wa Gaza. Mlipuko huo pia ulisababisha kukatika kwa umeme hali iliyoathiri zaidi muunganisho wa mtandao. Mashambulizi hayo yalipiga mnara wa Al-Jawahra mnamo Mei 12 na kuathiri miundombinu ya mawasiliano ya simu katika jengo hilo. Mnamo Mei 15, shambulio hilo liliangusha mnara wa Al-Jalaa[109] ambao una ofisi za baadhi ya watoa huduma za mawasiliano na mashirika ya vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na Associated Press na Al Jazeera. Fusion, kampuni ya mawasiliano ya eneo hilo iliripoti kukatizwa kwa huduma zake kutokana na milipuko ya mabomu mnamo Mei 12, 14, na 18.[110] Uharibifu huu ulizima sauti za Wapalestina. Wapalestina walipoweza kuunganishwa, majukwaa makuu kama Facebook na Instagram yaliondoa

103 Abiy Ahmed Ali. Facebook post. July 18, 2021. Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://web.facebook.com/112704996810839/posts/573861097361891/.

104 Rest of World (2021). *Why Facebook keeps failing in Ethiopia.* Imerejeshwa Machi 23, 2022, kutoka https://restofworld.org/2021/why-facebook-keeps-failing-in-ethiopia/.

105 Ibid.

106 Ibid.

107 CNN (2021). *Facebook knew it was being used to incite violence in Ethiopia. It did little to stop the spread, documents show.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://edition.cnn.com/2021/10/25/business/ethiopia-violence-facebook-papers-cmd-intl/index.html.

108 BBC News (2021). *Facebook deletes Ethiopia PM's post that urged citizens to 'bury' rebels.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://www.bbc.com/news/world-africa-59154984.

109 SMEX (2021). *Israeli Airstrikes Destroyed Internet Infrastructure In Gaza [Report].* Imerejeshwa Februari 28, 2022, kutoka https://smex.org/israeli-airstrikes-destroyed-internet-infrastructure-in-gaza-report/; Internet Outage Alerts (@gatech_ioda). Twitter post. 3:59 pm. May 16, 2021. Imerejeshwa Februari 28, 2022, kutoka https://twitter.com/caida_ioda/status/1393959216595959810.

110 Fusion Internet and Communications Services (@FusionGaza). Facebook post. May 12, 2021. Imerejeshwa Februari 23, 2022, kutoka https://web.facebook.com/FusionGaza/posts/4399068443459303.

machapisho yao na kusimamisha akaunti zao chini ya sera na kanuni za upendeleo ambazo kwa ufanisi kama si kwa makusudi ziliwadhibiti.[111]

## Mapinduzi ya kidijitali ya jeshi la Myanmar yanayoendelea

Mnamo Februari 1 2021, wakati jeshi lilipoanzisha mapinduzi nchini Myanmar, jeshi lilifunga njia nyingi za mawasiliano kwa muda wa nusu siku nchini kote katika jaribio la kudhibiti kuenea kwa habari kuhusu mapinduzi na kuwezesha kukamatwa kwa wanachama muhimu wa jeshi, upinzani wa kisiasa na asasi za kiraia.[112] Hii ilijumuisha kukata ufikiaji wa mtandao, mitandao ya simu za rununu, idhaa za redio na vituo vya televisheni - isipokuwa chaneli ya televisheni ya Myawaddy inayomilikiwa na jeshi.[113] Mnamo Februari 3, jeshi lilirejesha ufikiaji wa simu za 4G katika baadhi ya vitongoji vya jimbo la Rakhine, ambapo mtandao ulikuwa umesimamishwa kwa muda mrefu ili kuficha ukiukwaji wa haki za binadamu - labda ili kuvuruga tahadhari kutoka kwa mapinduzi. Kuzimwa kwa mitandao kulianza tena Februari 6 na 7, wakati junta ilikata ufikiaji wa mitandao nchi nzima kwa mara ya pili kwa takribani masaa 30 na kuzuia majaribio ya raia kupata habari sahihi kuhusu matukio yanayoendelea. Mamlaka ya kijeshi iliweka kizuizi kingine nchini kote mnamo Februari 15, na kuathiri mtandao wa nyuzi, mitandao isiyotumia waya na simu. Baada ya hapo, serikali kuu iliweka vizuizi vya mtindo wa kutotoka nje kila usiku kati ya saa 07:00 usiku na saa 03:00 asubuhi. Usumbufu huu wa usiku uliendelea hadi Aprili 28. Aidha Machi 15, junta ilifunga huduma za mitandao wa simu kitendo ambacho kilikuwa na athari kubwa kwa sababu watumiaji wengi wa mitandao nchini Myanmar wanategemea simu zao za mkononi kwa upatikanaji huo. Kufikia Aprili 1, Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano ilikuwa imeamuru watoa huduma za mitandao kusimamisha huduma za mtandao wa intaneti zisizotumia waya pia,[114] na hivyo kuongeza udhibiti wa wanajeshi kwenye intaneti. Ingekuwa miezi miwili na nusu kabla ya junta kurejesha muunganisho wa nyuzi na kurejesha muunganisho wa kebo, na hata hivyo ilifanya hivyo kwa "kuorodhesha" mashirika, makampuni na watu binafsi ambao muunganisho wa intaneti kwao ungesalia bila kukatizwa haswa.[115] Kuruhusu kuorodhesha kwa ufanisi hupindua dhana ya mtandao huru na wazi na hivyo kufanya kuzuia kawaida na kufikia kwa matabaka, kwa njia ya kibaguzi ambayo inazidisha ukosefu wa usawa hasa katika muktadha wa mapinduzi na mgogoro wa kibinadamu.

Ingawa jeshi lilirejesha ufikiaji wa mtandao hatua kwa hatua nchini kote mnamo mwaka 2021, bado linaendelea kuzima mtandao wa kikanda hadi leo, haswa katika maeneo ambayo wanajeshi wanakabiliana na upinzani.[116] Kuzimwa huku kwa mitandao ni majaribio ya wazi ya kuficha ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na ule unaoweza kusababisha uhalifu wa kimataifa.[117] Kwa kuongezea, junta imeendelea kupiga marufuku tovuti ikiwa ni pamoja na mitandao ya kijamii inayotumiwa sana na majukwaa ya ujumbe na kuwalazimisha watu nchini Myanmar kutumia VPN kupata ufikiaji wa mtandao. Ikiwa serikali ya kijeshi itatumia muswada wa usalama wa mtandao uliofufuliwa hivi majuzi matumizi ya VPN yataharamishwa.[118]

**111** The Washington Post (2021). *Facebook's AI treats Palestinian activists like it treats American Black activists. It blocks them.* Imerejeshwa Februari 23, 2022, kutoka https://www.washingtonpost.com/technology/2021/05/28/facebook-palestinian-censorship/.

**112** *Angali supra noti* ya 20.

**113** Radio Free Asia (2021). *News Stations Still Closed in Myanmar, Some Other Channels Reopen.* Imerejeshwa Februari 18, 2022, kutoka https://www.rfa.org/english/news/myanmar/stations-02022021181731.html

**114** Reuters (2021). *Myanmar orders wireless internet shutdown until further notice: telecoms sources.* Imerejeshwa Aprili 26, 2022, kutoka https://www.reuters.com/article/us-myanmar-politics-internet/myanmar-orders-wireless-internet-shutdown-until-further-notice-telecoms-sources-idUSKBN2BO5H2.

**115** Access Now (2021). *#KeepItOn: Immediately reinstate internet access for all in Myanmar.* Imerejeshwa Februari 23, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/cms/assets/uploads/2021/05/KeepItOn_-Immediately-reinstate-internet-access-for-all-in-Myanmar_31-May-2021.pdf.

**116** VOA (2021). *In Post-Coup Myanmar, Citizens Fight to Get Online.* Imerejeshwa Februari 22, 2022, kutoka https://www.voanews.com/a/myanmar-citizens-fight-to-get-online/6250855.html.

**117** BBC News (2022). *Myanmar Rohingya violence is genocide, US says.* Imerejeshwa Machi 28, 2022, kutoka https://www.bbc.com/news/world-asia-60820215.

**118** Access Now (2022). *Analysis: the Myanmar junta's Cybersecurity Law would be a disaster for human rights.* Imerejeshwa Januari 27, 2022, kutoka
https://www.accessnow.org/analysis-myanmar-cybersecurity-law/

## 2.4 Kuzimwa kwa mitandao nyakati za mitihani

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumeona nchi duniani kote zikifunga mtandao ili kuzuia udanganyifu wakati wa mitihani ya shule, zikiwemo Algeria, Bangladesh, Ethiopia,[119] India, Irani, Iraqi, Jordani, Mauritania,[120] Sudani na Syria. Licha ya athari mbaya iliyothibitishwa ya kuzima kwa mtandao, nchi kadhaa za Mashariki ya Kati na kanda ya Afrika Kaskazini zimeendelea kutekeleza usumbufu huu mwaka hadi mwaka pamoja na mwaka 2021.

**Algeria** imekuwa ikiongoza kwa kuzima mtandao inayohusiana na mitihani tangu mwaka 2016, na mwaka 2021 haikuwa na ubaguzi kwa sheria hiyo. Mnamo Juni, mamlaka ya Algeria ilifunga mitandao kati ya saa 2:00 asubuhi na saa 6:00 mchana wakati wanafunzi 731,000 walipokuwa wakifanya mitihani yao ya kwanza ya kitaifa. Usumbufu huu uliendelea siku nzima,[121] zikipishana kati ya kukatika kabisa kwa mtandao wakati wa vipindi vya mitihani na msongamano mkubwa - kupunguza kasi - ya huduma kati ya vipindi, wakati wa mapumziko ya mchana na usiku mmoja. Mamilioni ya watu Algeria haswa wanaotegemea mitandao ya kijamii na intaneti kufanya kazi na kujimudu wameathirika pakubwa.[122] Mnamo mwaka 2020 pekee, Algeria ilipoteza karibu dola milioni 388 kwa sababu ya uzimaji wa mitandao unaohusiana na mitihani[123] na wataalamu wa Algeria wanakadiria hasara za kiuchumi za Dinar milioni 500 za Algeria kwa kila saa ya kuzima kwa mtandao nchini.[124] Kuzimwa kwa mitandao kunaendelea licha ya taarifa ya Rais wa Algeria Abdelmadjid Tebboune kwenye TV kwamba "hatavumilia tena" tabia hii.[125]

**Syria** iliendelea na utamaduni wake wa kuzima mitandao wakati wa mitihani ya kitaifa mwaka 2021, mazoea ambayo yamekuwa ya kawaida kama saa tangu mwaka 2016.[126]

Mnamo mwaka 2020, **Sudani** ilitatiza huduma za mitandao kwa saa tatu wakati mitihani ya kitaifa iliyopangwa ilipokuwa ikifanyika.[127] Mnamo mwaka 2021, mwendesha mashtaka wa umma wa Sudani aliamuru tena watoa huduma za mitandao kuzima miunganisho ya mitandao wa rununu kwa mitihani hii.[128]

Serikali zinazoweka usumbufu huu zimehalalisha matumizi yao kama hatua ya awali ya kuzuia wanafunzi kudanganya au kuvujisha maswali ya mitihani. Walakini, hata kama mbinu hizi zilikomesha udanganyifu, kuzima mitandao sio kipimo cha kukidhi lengo hilo. Kuzuia udanganyifu haipaswi kuhitaji kudhoofisha haki za binadamu.

---

119 The Guardian (2017). *Ethiopia turns off internet nationwide as students sit exams.* Imerejeshwa Aprili 21, 2022, kutoka https://www.theguardian.com/technology/2017/may/31/ethiopia-turns-off-internet-students-sit-exams.

120 Ifex (2019). *Mauritanian government authorises disruption of internet services and blocks social media platforms.* Imerejeshwa Aprili 21, 2022, kutoka https://ifex.org/mauritanian-government-authorises-disruption-of-internet-services-and-blocks-social-media-platforms/.

121 Ali Sibai (@alisibai). Twitter post. 4:47 pm. June 21, 2021. Imerejeshwa Februari 22, 2022, kutoka https://twitter.com/alisibai/status/1407017281922682901.

122 Echoroukonline.com (2021). *Millions of Algerians are out of work because of the baccalaureate.* Imerejeshwa Februari 22, 22, kutoka https://www.echoroukonline.com/%D9%85%D9%84%D8%A7%D9%8A%D9%8A%D9%86-%D8%A7%D9%84%D8%AC%D8%B2%D8%A7%D8%A6%D8%B1%D9%8A%D9%8A%D9%86-%D8%A8%D9%84%D8%A7-%D8%B9%D9%85%D9%84-%D8%A8%D8%B3%D8%A8%D8%A8-%D8%A7%D9%84%D8%A8%D9%83%D8%A7%D9%84%D9%84%D9%88%D8%B1%D9%8A%D8%A7-%D8%A8%D8%B3%D8%A8%D8%A8-%D8%A7%D9%84%D8%A8%D9%83%D8%A7%D9%84%D9%84%D9%88%D8%B1%D9%8A%D8%A7.

123 Digital Watch Observatory (2020). *Internet restriction during exam in Algeria cost nearly US$388 million.* Imerejeshwa Februari 22, 2022, kutoka https://dig.watch/updates/internet-restriction-during-exam-algeria-cost-nearly-us388-million.

124 Access Now (2021). *Internet shutdowns during exams: when MENA governments fail the test.* Imerejeshwa Februari 23, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/mena-internet-shutdowns-during-exams/.

125 YouTube Video (2020). Imerejeshwa Februari 23, 2022, kutoka https://www.youtube.com/watch?v=a7Oxp6aKiQw.

126 Dyn Research (2016). Imerejeshwa Februari 22, 2022, kutoka https://web.archive.org/web/20160815064635/http://research.dyn.com/2016/08/syria-goes-to-extremes-to-foil-cheaters/.

127 Access Now (2020). *Internet shutdowns in Algeria and Sudan: damaging practices during exceptional circumstances.* Imerejeshwa Februari 23, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/internet-shutdowns-in-algeria-and-sudan-damaging-practices-during-exceptional-circumstances/.

128 Sudanesehome.net (2021). *Directive from the Attorney General to stop internet service starting tomorrow.* Imerejeshwa Februari 23, 2022, kutoka https://sudanesehome.net/

# III. Mitindo na maendeleo mashuhuri katika 2021

## 3.1 Kuzima mitandao kwa muda mrefu

**Hali nne ambazo mitandao ilifungwa kwa muda mrefu zaidi na kusajiliwa mwaka wa 2021**

| | |
|---|---|
| **Siku 2026** | **6/12/2016 - 12/28/2021**<br>**Sehemeu ya ya (FATA) ilokuwa chini ya mamlaka ya kifederali nchini Pakistan** |
| **Siku 593** | **6/22/2019 - 2/3/2021**<br>**Jimbo la Rakhine, Myanmar** |
| **Siku 551** | **8/5/2019 - 2/5/2021**<br>**Jammu na Kashmir - India** |
| **Siku 539** | **11/4/2020 - Inaendelea**<br>**Tigray, Ethiopia** |

Katika nusu ya mwaka wa 2021, tayari tulikuwa tumeandika mwendelezo wa mwelekeo unaoharibu sana: baadhi ya serikali zinarefusha kuingiliwa kwao kwa mitandao, na hivyo kuzidisha madhara makubwa waliyonayo kwa maisha ya watu.[129] Katika Maeneo ya Kikabila Yanayosimamiwa Kiserikali ya Pakistani yaani Federally Administered Tribal Areas(FATA), Mamlaka ya Mawasiliano ya Pakistani ilizuia mitandao kamili ya simu kufuatia mzozo katika mpaka wake na Afghanistani mnamo Juni 2016. Mitandao haikurejeshwa kikamilifu hadi Desemba 2021, na hivyo kuudisha maendeleo ya kiuchumi na kielimu miongo kadhaa nyuma kwa watu wanaoishi katika eneo ambalo tayari limetengwa.[130] Katika eneo la India la Jammu na Kashmir, watu wameteseka kwa kufungwa kwa mitandao kwa muda mrefu zaidi kwenye rekodi kulingana na nyaraka zetu. Lakini wenye mamlaka hawakuishia hapo. Waliendelea kulazimisha kuzima mitandao mara kwa mara na usumbufu wa mara **85** uliorekodiwa kwa jumla mnamo mwaka 2021 - na kuacha idadi ya watu katika hali ya muunganisho ulioathiriwa. Vile vile, nchini Ethiopia eneo la Tigray limezimiwa mitandao tangu Novemba 2020: hiyo ni miezi **18** na kuendelea. Huko Myanmar, watu katika vitongoji katika jimbo la Rakhine - lenye watu wengi wa makabila yaliyotengwa - wamepata hali ya kuzimiwa kwa mitandao kwa miaka mingi tangu 2019, kama tulivyoripoti katika ripoti yetu ya mwaka 2020.[131] Mitandao ilivyorejeshwa tu kwa watu wa eneo hilo, nchi nzima ilizima mitandao kwa sababu ya mapinduzi ya kijeshi.[132]

## 3.2 Kuongezeka kwa matumizi ya kuzima kwa simu wakati wa maandamano

Mnamo mwaka 2021, serikali **18** zikiwemo Bangladesh, Burkina Faso, Chadi, Cuba, Eswatini, India, Indonesia, Irani, Iraqi, Jordani, Kazakhstani, Myanmar, Pakistani, Senegal, Sudani ya Kusini, Sudani, Turkmenistani na Uganda, ziliweka vikwazo vya kuzima mitandao ya simu wakati wa maandamano. Kupunguza ufikiaji wa rununu ili kukabiliana na maandamano ni hali inayoongezeka ulimwenguni na angalau matukio ya kuzima simu **37** mnamo 2021 yaliathiri huduma za mtandao wa simu wakati wa maandamano ikilinganishwa na matukio **15** katika mwaka uliopita. Huku watu wengi zaidi wakigeukia

129 Access Now (2021). *#KeepItOn update: who is shutting down the internet in 2021?* Imerejeshwa Februari 23, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/who-is-shutting-down-the-internet-in-2021/.

130 Digital Rights Monitor (2021). *Mobile Internet Restored in Former FATA's Kurram Agency.* Imerejeshwa Aprili 20, 2022, kutoka https://www.digitalrightsmonitor.pk/mobile-internet-restored-in-former-fatas-kurram-agency/

131 Access Now (2020). *Shattered dreams and lost opportunities: A year in the fight to #KeepItOn.* Imerejeshwa Aprili 20, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/keepiton-2020-report.

132 The Irrawaddy (2021). *Mobile Internet Connectivity Restored to Western Myanmar.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.irrawaddy.com/news/burma/mobile-internet-connectivity-restored-western-myanmar.html#.


simu zao za rununu ili kufikia mitandao na majukwaa ya mawasiliano ya kidijitali duniani kote, na hasa katika nchi zinazoendelea na zinazoinukia,[133] watendaji wa serikali wametambua kuzima kwa mitandao wa simu kama njia muafaka ya kuwanyamazisha watu bila kulazimika kupeleka nchi nzima nje ya gridi ya taifa. Mbinu hii hasa ni ya kibaguzi na yenye madhara. Ingawa watu wanaoweza kumudu au kufikia chaguo ghali zaidi ili kupata mtandao, kama vile huduma za kebo zisizobadilika wanaweza kubaki wameunganishwa, watu na jumuiya zisizo na fursa kama hizo hazijumuishwi na kukatizwa na huduma. Hupanua mgawanyiko wa kidijitali kati ya walio na fursa, kama vile maafisa wa serikali, makampuni ya benki, wasomi, na kila mtu mwingine. Mamlaka zinaweza pia kulenga huduma za simu kwa kujaribu kuwanyamazisha wakosoaji wao ambao wanaweza kupata na kushiriki maelezo kwa faragha, na kuungana ili kupanga, kwa kutumia majukwaa au programu fulani za simu kama vile programu za mitandao ya kijamii, programu salama za kutuma ujumbe au VPN.

## 3.3 Uzuiaji unaolengwa wa majukwaa ya mawasiliano

Mamlaka zinazidi kujibu ukosoaji na upinzani wa umma kwa kuzuia mifumo mahususi ya mawasiliano. Baadhi ya serikali zilienda mbali zaidi na kukata ufikiaji wa VPN ambazo huwezesha watu kupita udhibiti.[134] Data yetu inaonyesha kuwa kukatizwa kwa huduma kulitokea katika nchi **22** katika mwaka wa 2021. Hii ni pamoja na Bangladesh, Uchina, Kuba, Eswatini, Ethiopia, India, Irani, Jordani, Kazakhstani, Myanmar, Nigeria, Omani, Pakistani, Russia, Senegal, Sudani ya Kusini, Sudani, Tajikistani, Turkmenistani, Uganda, Uzbekistani na Zambia.

Nchini **Myanmar** kwa mfano, jeshi liliwasukuma watoa huduma za mitandao kuzuia Twitter kama sehemu ya mapinduzi yake ya kidijitali. Uzuiaji huo ulitekelezwa kwa njia ambayo ilisababisha kile kinachoitwa "sumu ya kikoa," kumaanisha kuwa

**Kufungwa kwa mitandao vs kupunguzwa kwa huduma hizo**




**28**

**Katika hali zote zilizohusika, huduma kama mitandao ya kijamii huduma za kutuma risala mwakaa wa 2021**

- **Bila kufungwa, huduma kamili : 131**
- **Kuwa wazi lakini kwa huduma maalum 11**
- **Huduma pekee: 17**

iliathiri tovuti na huduma zisizohusiana kwa mbali kama Uhindi Magharibi.[135]

**Urusi** ilikaza Twitter kama sehemu ya vikwazo vyake vya mara kwa mara vya uhuru wa kujieleza, baada ya jukwaa kushindwa kuondoa mamlaka ya maudhui yaliyoripotiwa kuwa kinyume cha sheria. Kama tunavyoona hapo juu, msisimko huu uliishia kupunguza kasi ya kufikia zaidi ya vikoa 40,000 vilivyo na t.co (jina la kikoa lililofupishwa la Twitter). Hiyo ilijumuisha tovuti za mashirika ya serikali nchini Urusi na majukwaa kama vile Google na Yandex.[136]

133 Pew Research Center's Global Attitudes Project (2020). *Communications Technology in Emerging and Developing Nations.* Imerejeshwa Machi 21, 2022, kutoka https://www.pewresearch.org/global/2015/03/19/1-communications-technology-in-emerging-and-developing-nations/.

134 Angalia, kwa mfano Radio Free Europe Radio Liberty (2021). *VPNs Are Not A-OK: Turkmen Internet Users Forced To Swear On Koran They Won't Use Them.* Imerejeshwa Aprili 20, 2022, kutoka https://www.rferl.org/a/turkmenistan-vpn-koran-ban/31402718.html.

135 Doug Madory (@DougMadory). Twitter post. 7:40 pm. February 5, 2021. Imerejeshwa Aprili 19, 2022, kutoka https://twitter.com/DougMadory/status/1357776166820728840.

136 TechCrunch (2021). *Russia is trying to throttle Twitter.* Imerejeshwa Machi 23, 2022, kutoka https://techcrunch.com/2021/03/10/russia-is-trying-to-throttle-twitter/.


Nchini **Pakistani**, mamlaka ilikata ufikiaji wa majukwaa kadhaa makubwa ya mitandao ya kijamii ikiwa ni pamoja na Facebook, Twitter na TikTok kabla ya maandamano yaliyopangwa dhidi ya serikali.[137]

Wakati watu nchini **Irani** walihama kutoka WhatsApp hadi kwenye programu salama ya kutuma ujumbe, Signal kwa ajili ya faragha bora na uhuru kutoka kwa ufuatiliaji, mamlaka iliizuia. Mamlaka pia ziliamuru iondolewe kwenye Cafe Bazaar, toleo la Irani la Google Play na Myket, duka lingine la programu la ndani.[138] Signal ni moja tu ya jukwaa la hivi majuzi ambalo Irani imezuia. Serikali tayari imezuia Facebook, Twitter, YouTube na Telegram na hapo awali ilikuwa imezuia Signal mara kwa mara katika mwaka 2016 na 2017.

Vile vile nchini **Uchina**, Signal ikawa sehemu ya orodha ndefu ya mifumo ya kidijitali iliyozuiwa kwa muda usiojulikana na mamlaka mnamo Machi 2021 baada ya kuona ongezeko la idadi ya programu zinazopakuliwa.[139]

Lengo lingine la kuzuia lilikuwa Clubhouse, mtandao wa kijamii unaohusishagumzo ya sauti ya ambao watu hutumia kwa mijadala ya mitandaoni. Mnamo Machi 2021, mamlaka nchini **Jordani** ilizuia programu hiyo,[140] na wanahabari, wanaharakati na wengine walikimbilia kwenye mifumo mbadala kulaani uzuiaji huo kama matumizi mabaya ya wazi ya uhuru wa kujieleza na kupata haki za habari. Mwandishi wa habari wa Jordani Basil Alrafaih alizungumza kwenye Facebook akisema, "Mamlaka ambayo inaogopa kuzungumza na inayokandamiza watu wake ardhini na angani, haiwezi kukabiliana na janga."[141] Huko **Omani**, Idara ya Usalama wa Ndani iliiamuru Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano kuifungia Clubhouse kwa sababu ya ukosefu wa leseni ya kufanya kazi nchini.[142] Hilo lilizua maandamano kwenye Twitter kwa kutumia alama ya reli #Oman_bans_club_house.

**Kufungwa kwa majukwaa ya mawasiliano mwaka 2021**




**137** TechCrunch (2021). *Pakistan temporarily blocks social media.* Imerejeshwa Februari 23, 2022, kutoka https://techcrunch.com/2021/04/16/pakistan-temporarily-blocks-social-media/.

**138** Al Jazeera (2021). *Iran blocks Signal messaging app after WhatsApp exodus.* Imerejeshwa Februari 23, 2022, kutoka https://www.aljazeera.com/news/2021/1/26/iran-blocks-signal-messaging-app-after-whatsapp-exodus.

**139** Reuters (2021). *Encrypted messaging app Signal stops working in China.* Imerejeshwa Aprili 19, 2022, kutoka https://www.reuters.com/article/us-china-tech-signal/encrypted-messaging-app-signal-stops-working-in-china-idUSKBN2B8094.

**140** Jordan Open Source Association (2021). *Blocking Clubhouse in Jordan: A Quick Analysis of Internet Censorship Methods in Use.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://jordanopensource.org/blog/78/blocking-clubhouse-in-jordan-a-quick-analysis-of-internet-censorship-methods-in-use.

**141** RoyaNews (2021). *Jordan blocks Clubhouse application.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://en.royanews.tv/news/26508/2021-03-25.

**142** Access Now (2021). *Omani authorities block Clubhouse app.* Imerejeshwa Machi 24, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/clubhouse/.

Lakini labda mfano uliofungua macho zaidi wa mtindo wa 2021 ulikuwa uzuiaji wa Twitter wa **Nigeria**. Baada ya Twitter kufuta ujumbe wa Twitter wa Rais wa Nigeria Muhammadu Buhari akitishia mauaji ya halaiki kwa raia wa Nigeria Kusini, serikali ilifunga jukwaa kwa muda wa miezi saba kamili.[143] Kitendo hiki kilizua shutuma nyingi nchini Nigeria na duniani kote na kusababisha watu wengi nchini na nje ya nchi kutumia hashtag ya #KeepItOn kwenye Twitter kuangazia uzuiaji huo. Mamlaka zilijaribu kuwazuia Wanaijeria kukwepa kizuizi hicho kwa kutishia kuwafungulia mashitaka. Hii ilihamasisha mashirika ya kiraia kupinga uzuiaji huo mbele ya Mahakama ya Haki ya ECOWAS (Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi), kesi ambayo bado haijahukumiwa.[144]

## 3.4 Teknolojia zinazoendelea: kuchanganya kubana, kuzuia na kuzimwa kwa mitandao

Mnamo mwaka 2021, tuligundua matukio **10** ya kubana mitandao, **matano** kati ya hayo yalifanyika kwa wakati mmoja au kuingiliana na aina nyingine ya kuzima mitandao. Kubana ni kitendo cha kuzuia kiholela, lakini si kusimamisha mtiririko wa data kupitia mitandao ya mawasiliano. Kubana kunaifanya ionekane kana kwamba ufikiaji wa mitandao au jukwaa au huduma unapatikana, lakini kiwango cha uingiliaji kinatosha kufanya huduma au rasilimali kutokuwa na maana. Baadhi ya serikali ambazo ziliamuru kuzimwa mitandao kama vile Jordani, Urusi na Uganda zilitumia kubana mitandao kwa pamoja na vizuizi vingine vya huduma na athari ya kuongeza muda wa kuzima mtandao. Mchanganyiko kama huo wa teknolojia za kutatiza mawasiliano hufanya watu wasiweze kupata taarifa au kushiriki video au picha za ukiukaji wa haki za binadamu. Serikali zingine ambazo zilipunguza ufikiaji mnamo 2021 ni: Algeria, India, Irani, Iraqi na Myanmar.

Kumbuka: Katika sehemu nyingi za dunia, kutokana na miundombinu duni ya mitandao, inaweza kuwa vigumu kutofautisha kati ya kubana kimakusudi na miunganisho ya polepole ya intaneti. Kwa hivyo kubana kunaweza kuwa njia ya "kuficha" kuzimwa kwa mitandao kwa macho wazi. Hii inaweza kuwa sababu moja ya serikali nyingi kugeukia kubana mitandao: inaweza kuonekana kama tatizo la kiufundi au kushindwa kwa miundombinu, hata kama sababu halisi ni kukandamiza maandamano au kuingilia uchaguzi.

## 3.5 Kuzimwa mitandao kwa kulenga kwa maeneo na ya watu maalumu

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, tumeona serikali zikilenga kuzima huduma kwa mikoa mahususi, maeneo, na hivi majuzi hata majaribio ya kunyima ufikiaji wa mitandao kwa watu mahususi.[145] Mnamo mwaka 2021, matukio ya kuzimwa kwa mitandao **118** kati ya jumla ya **182** yaliyowekwa na serikali yaliathiri eneo moja au maeneo pekee ndani ya jimbo au mkoa huo. Ingawa kuzima mitandao kwa walengwa zaidi kunasikika kama hakutakuwa na madhara kidogo, mara nyingi ni ishara kwamba serikali inajaribu kunyamazisha idadi fulani ya watu ikiweka pembeni zaidi jamii ambazo tayari ziko hatarini.[146] Kuzimwa huku kwa mitandao kwa kulenga maeneo au watu pia kunaelekea kudumu kwa muda mrefu na kuwa na athari mbaya kwa haki za binadamu za wale wanaoishi katika vivuli, waliotenganishwa na mtu mwingine na ulimwengu wote.

143 Access Now (2021). *Blocking access to Twitter in Nigeria is a flagrant violation of fundamental rights.* Imerejeshwa Februari 23, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/nigeria-blocks-twitter-keepiton/.

144 Media Rights Agenda (2021). *ECOWAS Court Dismisses Nigerian Government's Motion to Strike out Suits over Twitter Ban, Sets May 10 for Judgment.* Imerejeshwa Februari 23, 2022, kutoka https://mediarightsagenda.org/ecowas-court-dismisses-nigerian-governments-motion-to-strike-out-suits-over-twitter-ban-sets-may-10-for-judgment/.

145 *Angalia supra* noti ya 46.

146 Media Matters for Democracy (2021). *Feminist Case Studies on the - Digital Rights Monitor.* Imerejeshwa Aprili 20, 2022, kutoka https://www.digitalrightsmonitor.pk/wp-content/uploads/2021/01/Women-Disconnected-Gender-Digital-Divide-in-Pakistan.pdf; PRIF BLOG (2022). *Internet Shutdowns in Ethiopia: The Weapon of Choice.* Imerejeshwa Aprili 20, 2022, kutokka https://blog.prif.org/2022/03/11/internet-shutdowns-in-ethiopia-the-weapon-of-choice/.

# IV. Kupambana katika mwaka 2021: changamoto na fursa

Kuzimwa kwa mitandao hutokea kwa sababu serikali zinataka kudhibiti mtiririko wa taarifa mitandaoni bila kujali matokeo yatakayowakumba watu wao wenyewe, uchumi na sifa zao duniani kote. Tamaa hiyo ya udhibiti imechangia kuongezeka kwa matumizi ya kukatizwa kwa mitandao, hata tunapoona kasi ikiongezeka katika mapambano ya kimataifa ya kukomesha kuzima mitandao. Ufuatao ni muhtasari wa baadhi ya maendeleo tuliyoyaona mwaka 2021 licha ya ongezeko na kuenea kwa usumbufu.

## 4.1 Hatua zilizopigwa katika ngazi za kimataifa

**Matamko ya G7 yalaani kuzima kwa mitandao:** Mnamo Mei 2021, washiriki katika Mkutano wa Mawaziri wa Mambo ya Nje na Maendeleo wa G7 walitoa taarifa ya kulaani "vitendo vya mataifa kuharibu kwa makusudi ufikiaji wa watu wao wenyewe kwa, au usambazaji wa habari, maarifa na data mitandaoni."[147] Wakuu wa nchi waliunga mkono maoni haya katika Taarifa yao wenyewe ya Mkutano wa Carbis Bay G7,[148] wakisema, "Pia tunathibitisha upinzani wetu kwa hatua ambazo zinaweza kudhoofisha maadili haya ya kidemokrasia, kama vile kuzimwa kwa mitandao na serikali na vizuizi vya mtandao." Hasa, taarifa hii ilikubali ufafanuzi wa kuzimwa kwa mitandao wa Access Now na wanachama wengi wa matumizi ya muungano wa #KeepItOn, inayoangazia ujuzi, kampeni na malengo yetu, na uwepo wetu katika matukio ya kuelekea Mkutano wa G7 wa 2021.

**Mtaalamu wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za kukusanyika na kujumuika kwa amani anaeleza njia ya kukomesha kuzimwa kwa mitandao**: Mtoa habari Maalum Clément Voule aliwasilisha *Kukomesha kuzimwa kwa mitandao: njia ya kuelekea* Kikao cha 47 cha Baraza la Haki za Kibinadamu mnamo Juni 2021, kama ufuatiliaji wa ripoti ya mwaka 2019 kuhusu haki za uhuru wa kukusanyika kwa amani na kujumuika katika enzi ya kidijitali.[149] Mtaalamu Maalum anataja kazi ya Access Now na ya muungano wa #KeepItOn,[150] kufafanua "ukubwa na ukali wa kuzimwa kwa mitandao kama njia ya kukandamiza haki ya kukusanyika kwa amani." Pia anatoa mfululizo wa mapendekezo kwa watendaji wa serikali, makampuni, wawekezaji na mashirika ya kimataifa ili kubadili mwelekeo huu mbaya.[151]

**Azimio la Umoja wa Mataifa linalaani kuzimwa kwa mitandao na linataka ripoti kuhusu kukatizwa:** Wakati Baraza la Haki za Kibinadamu la Umoja wa Mataifa lilipopitisha toleo jipya la azimio la "kukuza, kulinda na kufurahia haki za binadamu kwenye Mitandao" (A/HRC/47/16 ) mnamo Julai 2021,[152] ilitoa wito mahsusi wa kutozima mitandao na kuamuru ripoti kuhusu "mwenendo wa kuzimwa kwa mitandao, kuchambua sababu zake, athari zake za kisheria na athari zake kwa haki anuwai za binadamu, pamoja na haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni." Access Now na washirika wetu walishawishi azimio hili na kuchangia ushahidi na uchanganuzi wa ripoti.[153]

**Jukwaa la kimataifa la wadau wengi linaanzisha kikosi kazi cha kimataifa cha kuzimwa kwa mitandao:** Mnamo Desemba 2021, katika

147 Access Now (2021). *G7 leaders decry internet shutdowns, but leave personal data up for grabs*. Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/g7-internet-shutdowns-personal-data/.

148 G7UK.org (2021). *Carbis Bay G7 Summit Communiqué.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.g7uk.org/wp-content/uploads/2021/06/Carbis-Bay-G7-Summit-Communique-PDF-430KB-25-pages-5.pdf.

149 United Nations (2021). *Ending Internet shutdowns: a path forward. Geneva, Human Rights Council.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://undocs.org/A/HRC/47/24/Add.2

150 *Angalia supra* noti ya 131.

151 Kwa maelezo zaidi, Angalia Access Now (2021). *U.N. propels internet shutdowns into the spotlight, calls on key stakeholders to act.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/un-internet-shutdowns/.

152 United Nations (2021). *The promotion, protection and enjoyment of human rights on the Internet: resolution.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://digitallibrary.un.org/record/3937534?ln=en.

153 Access Now imeweka chombo cha ufuatilizaji wa ripoti kama hizo, kiitwacho "Relevant -to-KIO", ambacho kimechangiwa hadi mwisho wa zoezi na ambacho kinaweza kuonekana na watu wote kupitia http://accessnow.org/relevant-to-keepiton

mkutano wa Muungano wa Uhuru wa Mitandao (FOC), Access Now, Idara ya Jimbo la Marekani na Mpango wa Global Network ulizindua **Kikosi Kazi kipya cha FOC kuhusu Kuzimwa kwa Mitandao**.[154] Katika uzinduzi huo, vikundi hivi vilisisitiza wajibu wa FOC kuendeleza uhuru wa mtandao na kusisitiza umuhimu wa "kushiriki na kuendeleza rasilimali, kutoa kauli zinazolengwa na kuunda na kutumia njia zinazoaminika za mawasiliano kati ya washikadau wote ili kuwezesha ushirikiano."[155]

## 4.2 Hatua Zilizopigwa mahakamani za kupinga kuzimwa kwa mitandao

Pamoja na changamoto ya kuongezeka kwa kuzimwa kwa mitandao Afrika mnamo mwaka 2021,ilikuja fursa ya kupambana na usumbufu huo mahakamani, kuanzisha kesi kisheria na kutengeneza sheria ya kesi dhidi yao - zawadi kwa wanaharakati wa mashirika ya kiraia, watetezi wa haki za binadamu na washikadau wengine duniani kote.

Tuliona changamoto muhimu za kisheria nchini Nigeria, Sudani, na Zambia.

**Nigeria**: Baada ya Twitter kutupilia mbali ujumbe wa Rais wa Nigeria Muhammadu Buhari, serikali ilikatiza ufikaji  Twitter.[156] Mashirika ya kiraia ikiwa ni pamoja na SERAP (Mradi wa Haki za Kiuchumi na Uwajibikaji) yaliwasilisha kesi katika Mahakama ya Haki ya ECOWAS. Mashirika ya kimataifa Access Now, Electronic Frontier Foundation na Open Net Association ziliunga mkono shtaka la SERAP[157] kupitia muhtasari wa pamoja usio na upendeleo.[158] Serikali ilijaribu na kushindwa kwa kesi hiyo kutupiliwa mbali na walalamikaji bado wanasubiri hukumu. Hasa, Mahakama ya Haki ya ECOWAS hapo awali ilitoa uamuzi dhidi ya kufungwa kwa mtandao Togo mnamo mwaka 2020,[159] ikithibitisha haki za kimsingi za watu walioathiriwa.

**Sudani**: Wakati mamlaka ya Sudani ilipokata ufikiaji wa mitandao mnamo Oktoba 2021, Shirika la Kulinda Wateja la Sudani liliishtaki Mamlaka ya Mawasiliano na Udhibiti wa Posta (TPRA).[160] Baada ya hakimu kuamuru kurejeshwa kwa ufikiaji wa mitandao mnamo Novemba 11, 2021,[161] TPRA ilipinga marejesho kwa misingi ya "usalama wa taifa" na "hali ya hatari"[162] hoja ambazo mahakama ilizitupilia mbali. Wakati makampuni ya mawasiliano nchini Sudani bado yalishindwa  wa mitandao, jaji alichukua hatua isiyokuwa ya kawaida ya kutoa hati ya kukamatwa kwa maafisa wakuu watendaji.[163] Hapo ndipo ufikiaji wa mitandao uliporejeshwa.[164] Ni jambo la kutia moyo  na la kupongezwa sana kwamba jumuia za kiraia za Sudani zimeitikia mwitikio wa matumizi ya kuzimwa kwa mitandao tangu 2019 kwa kuwawajibisha wasimamizi, serikali na watoa huduma za mitandao. Kama matokeo, tumeona maamuzi manne ya mahakama dhidi ya

**154** Freedom Online Coalition (2021). *Task Force on Internet Shutdowns (TFIS).* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://freedomonlinecoalition.com/task_forces_and_wg/task-force-on-internet-shutdowns/.

**155** Freedom Online Coalition (2021). *Openness, Accessibility and Inclusion - Human Rights* ... Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://freedomonlinecoalition.com/wp-content/uploads/2021/12/Freedom_Online_Conference_2021_Chairs_Summary.pdf.

**156** The New York Times (2021). *Nigeria Bans Twitter After President's Tweet Is Deleted.* Imerejeshwa Februari 22, 2022, kutoka https://www.nytimes.com/2021/06/05/world/africa/nigeria-twitter-president.html.

**157** Vanguard News (2021). *SERAP drags Buhari before ECOWAS Court over Twitter ban in Nigeria.* Imerejeshwa Februari 22, 2022, kutoka https://www.vanguardngr.com/2021/06/serap-drags-buhari-before-ecowas-court-over-twitter-ban-in-nigeria/.

**158** Access Now (2021). *Access Now to ECOWAS Court: overturn Nigeria's Twitter ban.* Imerejeshwa Februari 22, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/nigeria-twitter-ban-ecowas-court/.

**159** Media Defence (2020). *Landmark Judgment: ECOWAS Court Finds Togo Violated FoE with Internet Shutdown.* Imerejeshwa Februari 22, 2022, kutoka https://www.mediadefence.org/news/landmark-judgment-ecowas-court-finds-togo-violated-foe-with-internet-shutdown/

**160** Reuters (2021). *Sudan court orders restoral of internet, but no sign of services returning.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.reuters.com/world/africa/court-orders-restoration-sudan-internet-access-2021-11-09/.

**161** SMEX (@SMEX). Twitter post. 9:13 am. November 12, 2021. Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://twitter.com/SMEX/status/1459086911931363329.

**162** SMEX (@SMEX). Twitter post. 2:08 pm. November 11, 2021. Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://twitter.com/SMEX/status/1458798801079226371.

**163** شبكة مدونون سودانيون (@Sudaneseblogs). Twitter post. 9:48 am. November 18, 2021. Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://twitter.com/Sudaneseblogs/status/1461270116809781248.

**164** Khattab - خطّاب (@ga800l). Twitter post. 2:32 pm. November 18, 2021. Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://twitter.com/ga800l/status/1461341451745304577.

kuzimwa kwa mitandao Sudani.[165]

**Zambia**: Baada ya Chapter One Foundation kuwasilisha kesi mahakamani kupinga kuzuiwa kwa mitandao ya kijamii siku ya uchaguzi, Mahakama Kuu ya Zambia ilitoa uamuzi wa kihistoria kuamuru mamlaka kurejesha utendakazi wa mitandao kamili mara moja.[166] Katika uamuzi wa mahakama wa suluhu na idhini mnamo Machi 21, 2022, Mamlaka ya Habari na Mawasiliano ya Zambia (ZICTA) ilikubali kutochukua hatua nje ya mamlaka yake ya kisheria na/au kudhibiti kukatiza mtiririko au ufikiaji wa mitandao kuendelea. ZICTA pia ilikubali kutoa notisi kwa umma ndani ya saa 36 za kuzima kwa mtandao wowote.[167]

Kesi hizi za mahakama zinafaa: kesi za Zambia na Sudani zilikomesha kuzimwa kwa mitandao kwenye nchi hizo wakati mamlaka hazingekoma licha ya malalamiko ya umma. Sisi na washirika wetu tunasubiri kwa hamu hukumu ya kesi ya Nigeria.

## 4.3 Maendeleo ya kuwezesha asasi za kiraia kukwepa na kupinga kuzimwa kwa mitandao

Access Now na wadau wengine wa muungano wa #KeepItOn waliunda rasilimali kadhaa muhimu mwaka 2021, zote zimeundwa ili kuwasaidia watu kutazamia, kuvinjari na kuandika kuzimwa kwa mitandao ambako kunahujumu demokrasia yetu na kuharibu haki za binadamu.

**Uangalizi wa Uchaguzi 2021**: Katika Access Now, tulizindua mpango wa kuripoti chaguzi zijazo ambazo zinaweza kusababisha kuzimwa kwa mitandao, kutoa masasisho ya wakati halisi kuhusu kukatizwa na kuhimiza hatua za kusaidia #KeepItOn.[168] Kuzuia kuzimwa kwa mitandao wakati wa uchaguzi ni jambo la lazima duniani kote, kwani kunazuia watu kukaa na habari, kukagua chaguzi zao wenyewe na kuhakikisha uadilifu wa michakato ya kidemokrasia. Watu lazima wawe na uwezo wa kuandika makosa na kushiriki ushahidi na ulimwengu wote.

**Kitabu cha Mwongozo wa Kuzimwa kwa Mitandao na Uchaguzi wa #KeepItOn**: Aidha, tulizindua kitabu cha mwongozo kilicholenga waangalizi wa uchaguzi, balozi, wanaharakati na waandishi wa habari.[169] Kinaeleza kwa nini kuzimwa kwa mitandao ni kikwazo kwa uchaguzi wa kidemokrasia, na inatoa mapendekezo ya kuelekeza kuzima mitandao, ikiwa ni pamoja na maelezo kuhusu jinsi ya kutambua ishara za tahadhari za mapema, jinsi ya kujiandaa na kuepuka usumbufu na jinsi ya kufuatilia na kuandika kuzimwa kwa mitandao kunakotokea.

**Uangalizi wa Kuzimwa kwa Mitandao**: Kuhifadhi Nyaraka kwa Haki za Kibinadamu: Kampeni hii ya kimataifa ya WITNESS huwasaidia wanaharakati, watetezi wa haki za binadamu, mashahidi wa raia kwa macho, waandishi wa habari na waandishi wa makala kujiandaa mapema kuandika ukiukaji wa haki za binadamu wakati wa kuzimwa kwa mitandao.[170]

**Tayarisha, Zuia, Pinga: Mtiririko wa Kazi ya Utetezi wa Kuzimwa kwa Mitandao**: Imeundwa na Internews kwa ushirikiano na jumuia ya #KeepItOn na watafiti kote ulimwenguni, tovuti hii ndogo ni hazina ya ajabu ya jinsi ya kutetea kwa ufanisi dhidi ya kuzimwa kwa mitandao.[171]

Hizi ni baadhi tu ya rasilimali zilizotengenezwa mwaka 2021 ambazo zinaonyesha kuongezeka kwa hali ya kisasa na nguvu ya upinzani wa mashirika ya kiraia

165 CIPESA (2022). *Litigating Internet Disruptions in Africa: Lessons from Sudan.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://cipesa.org/2022/03/litigating-internet-disruptions-in-africa-lessons-from-sudan/.

166 AllAfrica.com (2021). *Zambia: High Court Orders Restoration of Internet Services.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://allafrica.com/stories/202108150063.html.

167 Business and Human Rights Resource Centre (2022). *Zambia: Telecom regulator agrees to inform public of reason for any interruption in access to internet within 36 hours of any such event in future.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.business-humanrights.org/en/latest-news/zambia-telecom-regulator-enters-into-a-consent-judgement-on-internet-shutdowns-agrees-to-inform-the-public-of-the-reason-for-any-interruption-in-access-to-internet-within-36-hours-of-any-such-event-in-future/.

168 *Angalia supra* noti ya 92

169 *Angalia supra* noti ya 10.

170 WITNESS Media Lab (2021). *Eyes on Shutdowns: Documenting for Human Rights.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://lab.witness.org/projects/internet-shutdowns/.

171 Internews (2021). *Prepare, Prevent, Resist - Information Saves Lives.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://internews.org/resource/optimashutdownworkflow/.

dhidi ya kuzimwa kwa mitandao kote ulimwenguni.

### 4.4 Maendeleo ya ufuatiliaji shirikishi na uchanganuzi wa kuzimwa kwa mitandao

Kupambana na uzimaji kwa mitandao kunahitaji juhudi za pamoja kutoka kwa watendaji mbalimbali duniani. Ufuatiliaji na uwekaji kumbukumbu matukio ya kuzimwa kwa mitandao bado ni muhimu kwa kutahadharisha umma na kuwawajibisha wahusika. Huku serikali zikizidi kuwa za kisasa zaidi katika kuweka vikwazo, na hivyo kufanya iwe vigumu kugundua hitilafu fulani, tunafurahia kukua kwa jumuia ya upimaji ya #KeepItOn mwaka wa 2021. Makampuni na mashirika kama Cloudflare,[172] Censored Planet,[173] Mozilla,[174] na RIPE Atlas[175] wamejitolea kutupa maarifa ya kiufundi na data juu ya kuzimwa kwa mitandao kunapotokea. Jigsaw ya Google inafuatilia kwa karibu kuzimwa kwa mitandao na imechapisha uchanganuzi wa kina unaoangazia athari za usumbufu huu kwenye haki za kimsingi duniani kote.[176]

Mikakati hii ni pamoja na kazi muhimu inayoendelea ya Open Observatory of Network Interference [Uchunguzi wa Wazi wa Kuingiliwa kwa Mtandao (OONI)],[177] Internet Outage Detection Analysis [Uchambuzi wa Utambuzi wa Kukatika kwa Mtandao (IODA)],[178] Measurement Lab (M-Lab),[179] na Internet Society Pulse[180] miongoni mwa zingine. Utofauti wa jumuia ya ufuatiliaji hufanya ufuatiliaji kuwa imara zaidi, kuzuia wahalifu kuficha mienendo yao.

## V. Hitimisho: harakati zetu zinahitaji kuendelea kukua

Tunapozingatia mwaka 2021 katika muktadha wa data ya miaka mitano iliyopita, tunaona mwaka unaoakisi changamoto inayoendelea ya kuzuia mamlaka za serikali, wale wanaohusika katika mizozo ya kijeshi na watawala wa kijeshi kutokana na kutumia kuzima mitandao kama zana za udhibiti. Jamii kote ulimwenguni zinapojitahidi kukaa salama na zenye afya wakati wa janga la COVID-19, ni wazi matokeo ya usumbufu ni mabaya - bila kujali muktadha au mantiki. Tunatarajia, tunapata msukumo kutokana na maendeleo ambayo muungano wa kimataifa wa #KeepItOn umekuwa ukifanya licha ya kuongezeka kwa usumbufu duniani, kuanzia kudorora kwa kukwama kwa uchaguzi duniani kote, changamoto za mahakama barani Afrika, ukuaji wa rasilimali na uwezo wa kufuatilia, kukwepa kuweka kumbukumbu matukio ya kuzimwa kwa mitandao. Tunatumaini kufanya maendeleo zaidi katika miaka ijayo na kujenga shinikizo ili kuzuia usumbufu wa mitandao ambao unasababisha madhara mengi. Tunakuhimiza ujiunge na vita.[181]

172 Cloudflare Radar (2021). *Working with those who protect human rights around the world.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://blog.cloudflare.com/working-with-those-who-protect-human-rights-around-the-world/.

173 Censored Planet (2021). *An Internet-wide, Longitudinal Censorship Observatory.* Imerejeshwa Machi 2022, kutoka https://censoredplanet.org/.

174 Data@Mozilla (2022). *Documenting outages to seek transparency and accountability.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://blog.mozilla.org/data/2022/03/09/mozilla-opens-access-to-dataset-on-network-outages/.

175 RIPE Labs (2022). *The Kazakhstan Outage - As Seen from RIPE Atlas*. Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://labs.ripe.net/author/emileaben/the-kazakhstan-outage-as-seen-from-ripe-atlas/.

176 Jigsaw (2021). *The Current: The Internet Shutdowns Issue.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://jigsaw.google.com/the-current/shutdown/.

177 OONI Explorer (2021). *Open Data on Internet Censorship Worldwide.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://explorer.ooni.org/.

178 IODA (2021). *Internet Outage Detection and Analysis.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://ioda.caida.org/.

179 MLab (2021). *Measurement Lab.* Imerejeshwa Machi 25, 2022, kutoka https://www.measurementlab.net/.

180 Internet Society Pulse (2021). *Internet shutdowns.* Imerejeshwa Aprili 17, 2022, kutoka https://pulse.internetsociety.org/shutdowns.

181 Access Now (2021). *#KeepItOn: Fighting internet shutdowns around the world.* Imerejeshwa Machi 22, 2022, kutoka https://www.accessnow.org/keepiton/.

## MAWASILIANO

Kwa maswali na maelezo zaidi, tafadhali tembelea:
https://www.accessnow.org/keepiton/

Au wasiliana na:

**Felicia Anthonio**
Meneja wa Kampeni wa #KeepItOn, Access Now
felicia@accessnow.org




# KURUDI KWA UBABE WA KIDIJITALI

**Kuzimwa kwa mitandao mnamo mwaka 2021**

#KeepItOn